JACKPOT BABA LAO!
TZS. 472,189,430
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mwekezaji** mzawa amwangukia Rais kumpatia hati anayodai kupokwa

UKURASA 3





UKURASA 9

Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Februari 12, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581219
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kicheko vyuoni

• **Rais** atangaza kuongeza posho ya kujikimu... *Ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu akizungumza na Viongozi wa Shirikisho la Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO) na ZAHLIFE la Zanzibar, baada ya kuwasili Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. Wa (nne kushoto) ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda. **PICHA: IKULU**

## Sheria ya kupeana figo yaja

UKURASA 2

## Wataka mkakati maalum kuajiri walimu sayansi

UK 3

MICHEZO YANGA KUWAMALIZA WATUNISIA MAPEMA UK. 24
MAONI, KATUNI UK.6

## Sheria kupeana figo yanukia

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kutunga sheria itakayoruhusu wananchi kuchangiana viungo vya ndani ya mwili ikiwamo figo.

Vilevile, imeitaka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa waadilifu kwenye sampuli zinazohusu ubakaji na vinasaba vya uhalali wa mtoto.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu aliyasema hayo jana jijini Dodoma kwenye hafla ya kuweka jiwe la msingi kwenye jengo la mamlaka hiyo.

Alisema Wizara hiyo inaona kuna ongezeko kubwa la magonjwa yasiyo ya kuambukiza hususani kwa vijana na watoto.

"Kuna ongezeko kubwa sana la magonjwa yasiyo ya kuambukiza, magonjwa ya kisukari, ya moyo, shinikizo la damu na saratani na magonjwa ya afya ya akili, bahati mbaya magonjwa haya ukiweza kuzingatia maelekezo ya wataalamu unaweza kuyadhibiti na usipofuata utaweza kuishi nayo na ni gharama kubwa.

"Kwa mfano, ukisafisha figo ni kati ya Sh. 180,000 hadi 200,000 kwa siku na bahati mabaya madaktari wetu wakiona una bima ya afya wanaweza kukuambia hata mara tano kwa wiki.

"Au upate mtu wa kukuchangia figo na Tanzania hatuna sheria ya kuchangia viungo, tunataka kuitunga," alisema.

Kuhusu uadilifu, Waziri Ummy alisema watumishi wa mamlaka hiyo wanapaswa kuwa waadilifu na kutenda haki wanaposhughulikia sampuli za jinai na ubakaji na za kupata uhalali wa mtoto.

"Ninaomba tuwe waadilifu, kwa mama haina shida maana mtoto anakuwa tumboni kwake lakini kwa baba ni shida na watoto wanateseka huku mtaani, wanaume wengi wanatelekeza watoto," alisema.

Aliishauri mamlaka hiyo kutoa elimu kwa jamii namna njema ya kutumia huduma za mamlaka hiyo katika kutafuta haki kwenye masuala ya familia na uzazi.

Kadhalika, Ummy alitaka mamlaka hiyo kuangalia namna ya kusaidia kupima uchafuzi wa mazingira wa kelele na mitetemo ambayo imekuwa tatizo kubwa kwa sasa.

Awali Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo na Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko alisema ujenzi wa jengo hilo ni mwitikio wa serikali wa kuhamia Dodoma na kupanua wigo wa huduma za mamlaka na limejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 8.1.

Alisema jengo litakuwa na maabara nane za vinasaba vya binadamu, maabara ya vinasaba vya wanyama na wanayamapori, sumu, microbiology na bidhaa za mazao na mazingira.



Dereva wa bodaboda akimsukuma dereva wa guta ili kumuongezea kasi ya mwendo katika Barabara ya Morogoro, eneo la Magomeni Mwembechai, Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Samia apeleka kicheko vyuoni

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan jana aliibua shangwe kwa viongozi wa serikali za wanafunzi wa vyuo vikuu alipoahidi kupandisha posho ya kujikimu kutoka Sh. 8,500 ya sasa hadi Sh.10,000 kwa siku.

Shangwe zilizoambatana na wimbo maalum wa kumpongeza 'mama', zilisikika Ikulu Rais alipotangaza neema hiyo kwa wawakilishi wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO) na Zanzibar (ZAHLIFE) kwenye viwanja vya Ikulu, Chamwino.

Rais Samia aliwataka wanafunzi kuwa na ufahamu kuhusu mwelekeo wa nchi na aina ya Taifa tunalotaka kulijenga ambalo linajitegemea kiuchumi.

"Suala la 'boom' (posho ya kujikimu), boom likimalizika mnapiga pasi ndefu, unakula mara moja kwa siku, Waziri wa Elimu, nenda kaangalie, tutaanza na 10,000," aliagiza Rais Samia na kuamsha shangwe kwa wawakilishi hao.

Aliwataka vijana wa vyuo vikuu kuelewa changamoto kubwa za kidunia zikiwamo mabadiliko ya tabianchi na usalama wa chakula na kutoa elimu kwa jamii kuhusu mikakati ya kukabiliana nazo.

Rais Samia pia aliwataka vijana kuwa mstari wa mbele kuielimisha jamii umuhimu wa kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji na kuwahimiza wananchi kuongeza

uzalishaji ili pia kunufaika na soko kubwa la bidhaa za chakula duniani.

Alisema walio wengi walizaliwa wakikuta tayari misingi ya nchi imeshawekwa, hivyo wana wajibu wa kusoma na kujua ilikuwaje, akijitolea mfano kwamba wakati anasoma, walikuwa wanafundishwa somo la Historia.

"Lakini sasa mitaala imekuwa ikibadilishwa mara somo hilo linaitwa Civics, mchanganyiko na ndiyo maana nikamwambia (Prof. Adolf) Mkenda kaeni tena mpitie upya mitaala tuone tunakwenda wapi, tunaelekea wapi na tuone tunawajengaje vijana wetu," alisema.

Rais Samia alisema katika kudhihirisha vijana ni taifa la leo, katika uteuzi wake wa mawaziri na wakuu wa wilaya, ameweka vijana wengi.

Alikumbusha kuwa wakati nchi inapata uhuru ilikuwa na chuo kikuu kimoja lakini sasa kuna vyuo vikuu 30. Kati yake, 12 ni vya serikali na 18 vya binafsi.

Alionya tabia ya kujilinganisha na mataifa makubwa yaliyoendelea, akisema: "Vijana wetu sasa hivi mnaangalia runinga, yaliyoko Marekani, Ulaya halafu mnasema 'ile ndiyo nchi, hapa kwetu basi tu, nchi gani hii ya kuishi'. Lakini ukienda Ulaya mtu anataka aje Tanzania akae maisha yote."

Alisema kujitegemea kunaanza na mtu mmoja mmoja, akiwasisitiza wasomi wanapohitimu kuwa mfano mzuri kwa jamii zinazowazunguka kutokana na elimu kubwa waliyoipata.

"Changamoto tuliyonayo ni kwamba mitaala yetu imebeba mambo mengi chungu mzima, bado kundi kubwa la vijana Watanzania hatukuwatayarisha kwamba wanapotoka vyuoni waweze kujiajiri.

"Lakini mwelekeo sasa ni huo, ndiyo maana tumetaka Wizara ya Elimu iangalie upya mitaala, tunataka mitaala itakayosomeshwa kuanzia sasa hadi huko mbeleni imtengeneze kijana akitoka aweze kujitegemea," alisema.

Rais alisema vijana wenye sifa ya kuingia vyuoni lakini wazazi wao hawana uwezo, serikali imezungumza na benki ikiwamo NMB iliyotenga Sh. bilioni 200 kwa ajili yao, kwamba wanaweza kukopa kwa riba nafuu kuwaendeleza watoto wao.

Alibainisha kuwa hatua nyingine inayochukuliwa na serikali ni kuzungumza na baadhi ya mataifa kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Pia alisema kuna watoto wa kitanzania 340 walioko mataifa mbalimbali ikiwamo China, Hungary, Misri na Morocco wanaonufaika na mfumo huo.

### MAADILI

Rais Samia pia alitumia hafla hiyo kuwaonya vijana na wananchi kwa ujumla dhidi ya utamaduni wa kigeni unaokwenda kinyume na maadili ya Kitanzania.

### WAZIRI MKENDA

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolfu Mkenda alisema miongoni mwa anayoyasimamia ni maelekezo ya Rais Samia aliyoyatoa kuhusu kuongezwa kwa mikopo ya elimu ya juu kutoka Sh. bilioni 464 hadi 570 kwa mwaka huu wa fedha, akiitaja ni nyongeza kubwa kuwahi kutokea tangu waanze kutoa mikopo hiyo.

Alisema jambo lingine ni kuweka usawa kwa udahili wa mwezi wa kwanza usishuke, akibainisha kuwa hadi sasa mikopo imefikia Sh. bilioni 654 na kufutwa kwa ada na faini kwa wanaoshindwa kurudisha mikopo.

Alitaja wanafunzi walionufaika na Samia Schoolarship kuwa ni takribani 640 ambao tayari wako vyuoni.

"Pia kuna dola milioni 100 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuwaendeleza kielimu wahadhiri wakiwamo wa vyuo vya sekta binafsi.

Aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya washiriki kikamilifu katika usimamizi wa ujenzi wa vyuo vya ufundi na kwamba wiki hii watapata picha kamili kuwa ni mkoa gani utahitaji mkandarasi, akimwomba Rais kusisitiza ili viongozi wote wajue kwamba ujenzi huo ni wao wote na wausimamie vizuri.

Rais wa TAHLISO, Frank Mkinda alimshukuru Rais Samia kwa kuwa mlezi mahiri anayejali watoto wake, akieleza kuwa miongoni mwa mafanikio waliyoyapata ni kuongezeka kwa bajeti ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Pia alimshukuru Rasi Samia kwa kutenga bajeti kubwa kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu ambayo kwa kiasi kikubwa imepunguza mzigo mzito wa gharama kwa wazazi wao.

"Moja ya vitu ambavyo vimetusaidia ni pamoja na kuondoa tozo ya kulinda thamani ya fedha kwa wanafunzi wanufaika wa mikopo ambao wanashindwa kumaliza kurejesha mikopo yao baada ya kumaliza masomo," alisifu.

Alisema mafanikio mengine ni kurudishiwa udahili wa wanafunzi kwa mwezi Machi, ambao alitaja kuwa umewekwa kwa ajili ya wanafunzi waliokosa vyuo mwezi Septemba na kwamba kwa kurudishwa kwa mfumo huo, kumetoa fursa kwa wanafunzi wengi wenye nia ya kujiunga na elimu ya juu.



Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya uchukuzi na biashara Iringa LTD, Caroline Mwakabungu akizungumza na waandishi wa habari, ofisini kwake mjini Iringa juzi, akimwomba Rais Samia Suluhu kuwasaidia kupata hati ya kampuni hiyo iliyochukuliwa mwaka 2019 na Tume ya uchunguzi wa mali za serikali wakati wa serikali ya awamu ya tano. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Wataka mkakati maalum wa kuajiri walimu wa sayansi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuweka nguvu maalum ya kuwaajiri walimu waliosomea masomo ya sayansi ili kuwa na idadi kubwa ya wanasayansi na wabunifu watakaochochea maendeleo ya taifa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi, Stanslaus Nyongo aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye hafla ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi.

Alisema Bunge linatambua umuhimu wa kumkomboa mtoto wa kike katika kumpatia elimu hasa elimu ya sayansi, hesabu na ubunifu.

"Wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi ni wachache sana, bado tuna changamoto kubwa hata katika ripoti yetu ya Kamati ya Bunge tulisema kwamba walimu wanaofundisha sayansi ni changamoto, ni wachache, tumeiomba serikali iweke nguvu maalum kuhakikisha inaweka mkakati wa kuwapata walimu wa sayansi hasa kuajiri walimu waliosomea masomo hayo ili wakafundishe kwenye shule zetu," alisema.

Nyongo alisema masomo ya sayansi na ubunifu ni muhimu kwa taifa, hivyo hakuna budi watunga sera na wapitishaji wa bajeti kuhakikisha zinatengwa fedha nyingi katika kumwendeleza mtoto wa kike kwenye sayansi na ubunifu.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga alisema maadhimisho hayo yana umuhimu wa kuhamasisha wanawake na wasichana kuwa wanasayansi ili kuchochea maendeleo ya nchi.

Alisema serikali inaendelea kuwekeza na kuwezesha miundombinu na rasilimali watu itakayowezesha kufanyika utafiti wa kisayansi wa kuzalisha ubunifu unaojibu kero za Watanzania ili kukuza sekta ya viwanda na za kipaumbele ifikapo 2025.

"Ubunifu wa wanawake na wasichana unahitajika na unachangia kikamilifu katika maendeleo hayo, tunafarijika sana kuona watanzania hasa wanawake na wasichana wanazalisha ubunifu mzuri," alisema.

Alitoa rai kwa wadau wa sekta ya umma na binafsi kuendelea kuunga mkono juhudi za wanasayansi wanawake na wasichana kuimarisha mchango wa utafiti na ubunifu wenye tija kwa ustawi wa uchumi kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Alitaja juhudi za serikali katika kuongeza mchango wa wanawake na wasichana kwa maendeleo ya nchi kupitia sayansi ni pamoja na utoaji wa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), ambayo inatoa kipaumbele kwa wanaojiunga kwenye fani za sayansi na pia uanzishwaji wa mfuko wa ufadhili wa Samia unaolenga kugharamia wanafunzi wa elimu ya juu wanaojiunga kwenye fani za tiba, uhandisi na hesabu.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23, wahitimu 640 wenye ufaulu wa juu kwenye mitihani ya kidato cha sita wamefadhiliwa kusoma programu za sayansi.

Alitoa wito kwa wazazi na jamii kuhamasisha watoto wa kike kupenda masomo ya sayansi na ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Awali Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Prof. Maulilio Kipanyula alisema takwimu zinaonyesha kuwa ni asilimia 24 pekee ya wanafunzi wa kike waliopo vyuoni, wanasoma masomo ya Sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati.

Mmoja wa wazungumzaji kwenye mdahalo wa ubunifu wa kisayansi wa wanawake katika kuleta maendeleo ya nchi, Dk. Augustina Alexander alitoa wito wa kuwekwa mazingira wezeshi yatakayosaidia kufanya ubunifu ambao utafanywa kuwa biasharisha na kupelekwa sokoni.

Mtaalamu wa Hesabu, Dk. Triphonia Ngailo alisema kuna umuhimu wa wanafunzi kuipenda hesabu na kuondokana na dhana potofu kuwa ni ngumu kwa kuwa ni kama kitendea kazi.

# Mwekezaji amwangukia Samia kupata hati anayodai kupokwa

**Na Paul Mabeja,** IRINGA

MKURUGENZI Mtendaji wa Kampuni ya Uchukuzi na Biashara ya Iringa LTD, Caroline Mwakabungu amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwasaidia kupata hati ya kampuni hiyo anayodai kuchukuliwa mwaka 2019 na Tume ya Uchunguzi wa Mali za Serikali.

Caroline aliwasilisha 'kilio' chao hicho jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu alichokiita usumbufu na manyanayaso ambayo wamekuwa wakiyapata kutoka kwa wanasiasa na mamlaka mbalimbali za kiserikali.

Alisema anamwomba Rais Samia kumsadia kupata hati hiyo ambayo ilichukuliwa mikononi mwa marehemu baba yake, Dk. Lucas Mwakabungu aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi kwa madai kuwa wanakwenda kuikagua.

"Mwaka 2019 walikuja watu kutoka Tume ya Uchunguzi wa Mali za Serikali iliyoundwa wakati wa utawala wa Hayati Rais John Magufuli na kampuni hii awali ilikuwa mali ya serikali ikijulikana kama RETCO, lakini mzee wangu na wenzake walinunua wakati ule wa sera ya ubinafsishaji chini ya uongozi wa Hayati Rais (Benjamin) Mkapa.

"Walipokuja wakadai kuwa wao ni tume ya serikali ambayo inakagua mali za serikali kama ziliuzwa kihalali, baba alijaribu kugoma kutoa hati ile lakini walimwambia kama anakataa watampa kesi ya uhujumu uchumi, ikabidi aitoe lakini hadi leo hatujui ipo wapi kwani tumekwenda hadi Hazina wanadai hawajui ilipo," alidai,

Alisema kuwa kutokana na hali hiyo, hawajui nini hatima yao kwa kuwa kuchukuliwa kwa hati kumekuwa chanzo cha wao kupata usumbufu na vitisho kutoka kwa baadhi ya viongoi wa serikali kutaka waondoke katika kampuni hiyo kinyume cha utaratibu.

"Mimi ni mtoto wa marehemu, nilichaguliwa kama Mkurugenzi Mtendaji na mwanahisa ninayewakilisha hisa nyingi na ninayewakilisha kundi la watu wenye hisa nyingi kwenye kampuni, nimekuwa nikipata misukosuko mingi kutoka kwa watu mbalimbali kinyume cha Sheria ya Kampuni Binafsi.

"Hata hivi ninavyozungumza na ninyi hapa, ninayo barua ya Mkuu wa Mkoa ambayo inanitaka nikabidhi ofisi ndani ya saa 48 kwa kamati ambayo sijui hata imeundwa na nani na jambo la ajabu ni kwamba hii ni kampuni binafsi, inakuaje mamlaka za serikali zinaingilia kinyume cha sheria ya kampuni binafsi? Kuna siri gani nyuma ya pazia?" alihoji.

Alisema anamwomba Rais Samia kuingilia kati mgogoro huo kwa kuwa unakatisha tamaa kwa wawekezaji wazawa kinyume cha jitihada zake ambazo amekuwa akizifanya kuweka mazingira wezeshi hasa kwa wanawake.

Pia alisema kuchukuliwa kwa hati hiyo kumesababisha mambo mengi kukwama ikiwamo kushindwa kupata mikopo kwenye taasisi za fedha ili kufanya uwekezaji.

"Tunafanya kazi tukiwa hatujui nini hatima ya kampuni hii kwani toka kupokwa hati imekuwa haiendelei kwa kuwa tunashindwa hata kuingia ubia na wawekezaji wengine na kukopa fedha, hivyo kukosesha mtaji wa kujiendesha na kuikosesha mapato serikali," alisema.

Mwanasheria wa kampuni hiyo, Mpeli Mwabungu alisema wanaiomba serikali kuingilia kati sakata hilo kutokana na kuwapo alichokiita tabia ya baadhi ya viongozi kuingilia uamuzi kwa kutoa matamko ya kisiasa ambayo yanasababisha baadhi ya wapangaji wao kugoma kulipa kodi kwa madai kuwa hilo ni eneo la serikali.



Mwanafunzi wa kidato cha nne shule ya St. Mary's Mbezi Beach, Sia John akikabidhi kombe kwa Mwenyekiti wa Bodi ya shule za St. Mary's, Dallas Mhoja, shuleni hapo, Dar es Salaam jana, walilopewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), baada ya kushika nafasi ya pili kwenye mashindano ya kujibu maswali kuhusu kodi, yaliyofanyika Chuo cha Kodi Mikocheni hivi karibuni. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Samia amefuta kilimo kuonekana sura ya matatizo, sasa kina mvuto

**Na Mwandishi Maalum**

KILIMO kilipewa sura ya matatizo. Kwa vijana ilionekana kufanya kilimo ni kazi isiyokuwa na staha, ilionekana ni jambo lisilolipa kiuchumi, lenye nafasi ndogo sana kwenye mafanikio. Hivyo, ushawishi wa vijana kuingia kwenye kilimo ulikuwa ni mdogo.

Malengo ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kilimo yameongeza mvuto wa kuwafanya vijana kukimbilia kilimo kuwa njia na daraja la ajira na kujiajiri na kuchukua njia sahihi ya kuwekeza kwenye kilimo na kufaidika na fursa zitokanazo na mnyororo wa thamani wa kilimo.

Mawazo ya Rais Samia ni kuzifanya serikali za mikoa na wilaya na taasisi zake kushiriki kwenye kilimo na kuona mchango wa kilimo katika uchumi wa viwanda.

Taasisi za serikali zichukue kwa vitendo na kuweka mazingira rasmi ya kilimo biashara kwenye maeneo yao.

Serikali ya awamu ya sita imefanikiwa kufanya kilimo kuwa kivutio na kichocheo cha ajira na uchumi kwa kuwavuta vijana wengi kushiriki kupitia Programu ya Building Better Tomorrow (BBT) itakayowasaidia kuwapa vijana mafunzo ya kuwaanda kuwa wakulima wakubwa wenye uzalishaji wenye tija.

Kupitia Programu ya BBT, serikali itachochea vijana kutoka mijini kwenda mashambani (vijijini) kwa kufungamanisha kilimo na maendeleo kupitia sekta binafsi kuifanya kuwa kichocheo cha uchumi wa nchi kuwa imara zaidi.

Serikali ya awamu ya sita imetoa fursa kuanzia uzalishaji wa mbolea na pembejeo ili kupunguza adha zitokanazo na gharama ya pembejeo.

Rais Samia ana imani vijana wanaweza kuinua kilimo kwa kutumia teknolojia mpya na ubunifu mpya. Vijana wa leo wana uwezo mkubwa kuzalisha fursa katika kilimo kupitia usanifu wa mashamba na upimaji wa udongo ili kilimo kisifanywe kwa kubahatisha.

Rais Samia amefanikiwa kwa uwezo mkubwa kufanya kilimo kuwa na mvuto, kimekuwa na sura yenye kulenga matarajio ya wengi hususani vijana.

Hilo limefanikiwa kupitia utoaji wa mikopo kwa vijana wanaoujihusisha na kilimo.

Rais amekifanya kilimo kupimika na kuwa na tija kwenye biashara, akiwaondolea mzigo kwa kuwasaidia kupata mikopo.

Rais pia amekuwa na mpango wa ugawaji wa mashamba kwa Vijana huku wakitafutiwa masoko ya bidhaa zenye uhitaji.

Ni wazi kuwa Rais Samia amezielewa changamoto za kilimo na amezitafutia ufumbuzi ili kijana aingie na kuwa na uhakika wa kufanikiwa.

Amekifungamanisha kilimo na teknolojia kupitia ugawaji wa vifaa vya kisasa kwa maofisa ugani wa kilimo nchi nzima, akisaidia kuwaunganisha kufanya mazingira ya usimamizi wa kilimo kuwa na njia rahisi kukusanya taarifa juu ya hali ya kilimo.

Serikali imetoa fursa ya kuwaingiza vijana kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi lengo la Rais Samia ni kuona vijana wanatumia rasilimali zilizopo katika uzalishaji wa mali.

Ni wazi kuwa lengo la Rais ni kutaka nchi kuwa hifadhi ya ya chakula ya nchi zinazotuzunguka na kuifanya nchi kuwa na uhakika wa chakula.

# TAF yalaani mauaji ya ofisa kilimo na askari

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

CHAMA cha Wataalamu wa Misitu Tanzania (TAF) kimelaani tukio la mauaji ya mtaalamu wa misitu na askari wa Jeshi la Akiba wawili waliokuwa doria kwenye msitu wilayani Uvinza mkoani Kigoma na kuitaka serikali kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wote waliohusika na mauaji hayo.

Rais wa chama hicho, Prof. Josiah Katani alitoa kauli hiyo jana jijini hapa aliposoma tamko la TAF kulaani tukio hilo la mauaji ya wataalamu wa misitu waliokuwa wakitekeleza majukumu yao.

Alikumbusha kuwa mnamo Januri 31 mwaka huu walipokea taarifa ya kuvamiwa na kushambuliwa kwa kikosi cha doria cha Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma kilichokuwa kikifanya doria kwenye hifadhi ya msitu wa Kijiji cha Chakulu.

Prof. Katani alisema kikosi hicho kilikuwa na jumla ya watu 22 na doria hiyo ilikuwa inaongozwa na Ofisa Misitu wa Wilaya ya Uvinza.

"Madhara yaliyotokea katika tukio lile ni pamoja na watu kuuawa eneo la tukio ambao ni ndugu Adam Ramadhani Harenga (Ofisa Misitu wa wilaya ya Uvinza) na MG 520961 Ibrahimu Seba Tokeo (askari wa Jeshi la Akiba).

"Aidha, Daniel Kalabamu ambaye ni Ofisa Utalii na askari wanne walijeruhiwa na kukimbizwa hospitalini," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na hali hiyo, TAF ilishitushwa na tukio hilo, hivyo kuitisha kikao cha pamoja cha dharura cha Kamati Tendaji ya chama hicho (NEC-TAF) na bodi ya wadhamini kilichofanyika Februari 4 mwaka huu na kuamua kutoa tamko hilo kupitia vyombo vya habari. "Matukio mengine kama haya ya kuuawa kwa wahifadhi wakiwa wanatekeleza majukumu yao yameripotiwa pia katika wilaya za Geita, Kasulu (Makere), Magu na Serengeti. Lakini matukio ya wafugaji kuingia maeneo yaliyohifadhiwa ni mengi na yanazidi kuongezeka," alisema.

Kiongozi huyo alisema chama hicho kinatoa masikitiko yake kwa tukio hilo lililotokea wilayani Uvinza na matukio mengine ya aina hiyo yaliyotokea huko nyuma kwenye maeneo mbalimbali nchini na kuwakumbuka wahifadhi.

"Chama cha Wataalam wa Misitu Tanzania kinalaani sana hatua ya wanaosemekana kuwa ni wafugaji wa mifugo kuwavamia wataalamu wa misitu na kujichukulia sheria mkononi ya kuwapiga kwa mawe na marungu na kusababisha majeruhi na vifo," alisema.

Aliongeza kuwa chama hicho kinaiomba serikali ichukue hatua kali za kisheria kwa wanaosemekana kuwa ni wafugaji waliohusika na tukio hilo la kikatili na kinyama ili kukomesha matukio hayo na iwe fundisho kwa wengine wanaojichukulia sheria mkononi pale wanapotakiwa kuondoka katika hifadhi walizovamia.

# Shule yang'ara shindano la TRA

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI wa Shule ya St Mary's Mbezi Beach jijini Dar es Salaam wameng'ara kwenye shindano la kujibu maswali mbalimbali yanayohusu kodi.

Shule hiyo ilishika nafasi ya pili ikitanguliwa na Shule ya Sekondari Kibaha ya mkoani Pwani katika shindano hilo lililofanyika kwenye Chuo cha Kodi Mikocheni mkoani Dar es Salaam.

Shindano hilo lililodumu kwa siku tatu, liliendeshwa hivi karibuni na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kushirikisha shule 59 za sekondari binafsi na za umma.

Akizungumzia shindano hilo jana, Mwenyekiti wa Bodi ya shule hizo, Dallas Mhoja alisema kufuatia ushindi huo, wanafunzi wa shule hiyo walizawadiwa kompyuta, mashine ya kudurufu, kombe na medali mbalimbali.

"Huwa tunashiriki mashindano mbalimbali yanayoandaliwa na TRA. mwaka huu tumeshiriki, zilikuwa shule 59 na katika hizo shule tulibuka washindi wa pili nyuma ya Kibaha iliyokuwa ya kwanza," alisema.

Alibainisha kuwa shindano hilo limefanywa na taasisi kubwa ya serikali kwa kushirikisha shule binafsi na za serikali, hivyo ushindi wa shule yao ni jambo la kujivunia kwa uongozi mzima wa shule.

Alisema wanafunzi wa shule hiyo walionyesha umahiri wa hali ya juu katika kujibu maswali mbalimbali yanayohusiana na kodi, hali iliyowafanya kuibuka wa pili.

"Kushindana na shule 59 za Mkoa wa Dar es Salaam, zikiwamo za binafsi na za serikali na kuibuka kwenye nafasi ya pili tunaona siyo jambo dogo kwetu. Tunajivunia mafanikio haya na mashindano yajayo tutashika namba moja," aliahidi.

Alitaja siri ya mafanikio hayo kuwa ni maandalizi mazuri ya wanafunzi na walimu wenye kuipenda kazi yao ambao wamekuwa wakifanya kazi usiku na mchana.

"Shindano hili limeleta msisimko mkubwa sana kwa wanafunzi wetu na walimu walioshiriki kwa sababu mbali na zawadi kama kompyuta, walizawadiwa fedha taslimu, hivyo mashindano haya ni muhimu sana," alisema.

HABARI KITAIFA

# Wanafunzi wa kike waona fursa ufundi

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WAKATI Dunia ikiadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi Februari 11 kila mwaka, wanafunzi wa kike wanaosomea masomo ya ufundi wamewataka wenzao wachangamkie fursa zilizopo kujiendeleza kwenye ufundi na kuondokana na dhana kuwa mafunzo hayo ni kwa ajili ya wanaume pekee.

Nipashe juzi ilitembelea vyuo mbalimbali vya mafunzo na ufundi, kikiwamo Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi, MVTTC na Mamlaka ya Elimu ya Ufundi VETA Kihonda na kuzungumza na baadhi ya wanafunzi wa kike wanaojifunza ufundi, wakisema wanajisikia fahari kujifunza mafunzo hayo.

Mmoja wa wanafunzi wa mwaka wa tatu wa VETA Kihonda, Mariam Ramadhani anayesomea kozi ya Agro Mechanics (utengenezaji wa zana za kilimo na kuzitumia), alisema:

"Tunaomba Serikali ituwezeshe sisi wanafunzi wa kike tunaosomea ufundi, itusaidie kupata ardhi, mbegu, mbolea, vifaa vya umwagiliaji ili tuwe mfano kwa wanawake wengine kwenye kilimo na utengenezaji wa zana za kilimo."

Alisema kilimo kipo wakati wote na teknolojia za kilimo zinakuwa siku hadi siku na wakulima wanaachana na jembe la mkono, hivyo ni vyema wakulima wakazidi kujifunza mbinu na teknolojia mpya kusaidia sekta hiyo.

Alisema kumwelimisha mwanamke ni kuelimisha taifa, hivyo ni vyema jamii wakiwamo wazazi, kuwapeleka watoto wa kike wajifunze zaidi masomo ya ufundi ambayo wanafundishwa kivitendo, wanapata ujuzi na ni rahisi kuajiriwa na kujiajiri kwa kuwa wanaaminika.

Wanafunzi wengine, akiwamo Sada Rashid anayesomea ujenzi mwaka wa pili VETA Kihonda, walisema kazi hiyo inafanywa na yeyote, hivyo watoto wa kike wasibweteke kwani wakifuzu, ni rahisi zaidi kupata kazi kulinganishwa na mwanamume.

"Tukipewa nafasi tunaweza, muhimu tujifunze. Mimi ninaweza ufundi kwa sababu kwanza ninajiamini, ni mdadisi, nina juhudi za kushawishi, kazi hizi hazitaki uvuvi, ninawaambia wanaolala nyumbani waondoke wakajiendeleze, wapunguze woga na dhana potofu kuwa kazi hizi ni za wanaume," alisema.

Petter Kadala ni Kaimu Msajili wa VETA Kihonda, alisema kupitia siku hiyo, wanaendelea kutengeneza mazingira rafiki ya kisayansi ili watoto wengi wa kike wajifunze na kupata ajira ama kujiajiri.

Alisema serikali imetengeneza mazingira rafiki kwa mtoto wa kike kujiajiri na kuajirika kwa kuweka sera nzuri zinazotoa fursa kwa watoto wa kike, hivyo ni vyema wazazi wakapeleka watoto wengi vyuo vya ufundi.

"Watoto wa kike wanaajirika haraka kwa sababu Serikali imeshaweka mazingira rafiki, ndio maana imeendelea kuongeza idadi vya vyuo vya mafunzo na jamii iondokane na dhana kuwa fani za ufundi ni kwa ajili ya watoto wa kiume, waachane nayo, wajue ni kwa ajili ya watoto wote," alisema.

Vijana wengine Sauda Rashid na Matruda David wanaosomea ufundi wa magari na umeme kutoka MVTTC, walisema ni vyema jamii ikatambua njia pekee ya kuondoa winbi la vijana wasio na ajira ni kuacha kuwakatisha tamaa vijana wa kike.

Walishauri jamii kuwapa fursa watoto wa kike kuonyesha ujuzi wao kwenye mafunzo na kazi zinazoonekana kushindwa kufanywa na wanawake ikiwamo ujenzi, umeme, ufundi bomba, ufundi magari, utengenezaji na uendeshaji wa mitambo ikiwamo mashine na kilimo.

# Tembo wavamia mashamba, waharibu mali

**Na Mwandishi Wetu,** NACHINGWEA

KUNDI la tembo limevamia mashamba ya wananchi katika kijiji cha Mwandila, kata ya Kiparemnero, Nachingwea mkoani Lindi na kusababisha athari kwa familia nne.

Tembo hao walivamia kijiji hicho na kuharibu mashamba hivyo kusababisha familia zilizoathirika kuhitaji msaada wa chakula.

Kutokana na uvamizi huo, Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo, alitembelea kaya hizo na kukabidhi msaada wa chakula wa kilo 120, yaani kilo 30 kwa kila familia ili kujikimu wakati hatua zingine zikichukuliwa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo juzi, Moyo alisema anafahamu changamoto hiyo inayotokana na uvamizi wa tembo katika mashamba na makazi ya wananchi.

Moyo alisema kutokana na hali hiyo, ameguswa kutoa msaada huo kwa familia ambazo hazina kabisa chakula.

Sambamba na hilo, alisema serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na wanyama hao ili kuhakikisha wananchi wanapata chakula pamoja na kuondokana na uvamizi huo wa mara kwa mara ambao umesababisha wakati mwingine vifo vya watu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwandila, Rajabu Chitanda, na Diwani wa Kiparemnero, Ally Milile, kwa nyakati tofauti walimshukuru mkuu wa wilaya kwa msaada huo huku wakiomba serikali kuendelea na jitihada zaidi kunusuru wananchi dhidi ya uvamizi huo.

Katika hatua nyingine, Moyo alifanya ziara kutembelea vikundi vya wajasiriamali waliopatiwa mkopo wa asilimia 10 halmashauri vikiwamo vikundi vya kuuza samaki, kubangua korosho na wauza matunda.

Moyo alivitaka vikundi hivyo kufanya kazi kwa bidii ili kupata pesa za marejesho na kuwezesha watu wengine wakopeshwe. Pia alikagua ujenzi wa barabara na kuagiza mkandarasi kukamilika haraka ujenzi na kumaliza kwa wakati kwa mujibu wa mkataba.

Tangu amehamia wilayani Nachingwea akitokea Iringa, Mkuu huyo wa wilaya amekuwa akifanya ziara kijiji kwa kijiji kukagua miradi na kujitambulisha kwa viongozi na wananchi.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo akikabidhi msaada wa chakula kwa mmoja wa wanafamilia wa kaya nne zilizoathirika na uvamizi wa tembo katika kijiji cha Mwandila, baada ya kuwatembelea akiwa katika ziara ya kijiji kwa kijiji kukagua miradi ya maendeleo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maofisa ugani wakabidhiwa pikipiki 200 kuinua kilimo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI imewataka maofisa ugani mkoani Shinyanga kuzitumia kwa madhumuni yaliyokusudiwa pikipiki za kilimo walizopewa na siyo kwenda kuzigeuza kuwa za biashara ya bodaboda.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yahaya Nawanda ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, alitoa angalizo hilo jana wakati akikabidhi pikipipi 221 kwa maofisa ugani wote wa mkoa huo.

Alisema serikali imetoa pikipiki hizo kwa maofisa ugani ili wakafanye kazi ya kutembelea wakulima na kuwapatia elimu ya kilimo cha kisasa na chenye tija kwa kuongeza uzalishaji wa mavuno na siyo kwenda kuzifanyia anasa.

"Tumewapatia pikipiki hizi maofisa ugani, nendeni kwa wakulima mkatoe elimu ya kilimo cha kisasa, kilimo chenye tija na kufanya kilimo biashara, hatutegemei kuona uzalishaji unashuka bali tunataka kuona uzalishaji wa mazao unakuwa mkubwa.

"Kazitunzeni pikipiki hizi vizuri ili zidumu muda mrefu na kufanya kazi ya kuwahudumia wakulima, msiende kuzifanya mambo ya anasa ikiwamo kufanya biashara ya bodaboda, zitumieni kwa mambo ya kheri," aliagiza.

Aliwataka maofisa ugani mkoani Shinyanga wawe na mashamba darasa angalau hata ekari moja, ili wakulima wapate kujifunza kwao na kufanya kilimo chenye tija kama ambavyo anafanya yeye huko mkoani Simiyu alikolima mashamba darasa ekari 10, tano za zao la pamba na tano za mahindi.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Shinyanga Mjini, Anold Makombe aliipongeza serikali kwa kuendelea kuimarisha sekta ya kilimo na kutoa pikipiki hizo kwa maofisa ugani.

Maofisa Ugani, akiwano wa Kishapu Godwine Evalist, walishukuru kupewa usafiri huo wa pikipiki ambao utawasaidia kuwafikia wakulima kwa wakati na kuwapatia elimu ya kilimo cha kisasa na kuongeza uzalishaji wa mavuno na kuinuka kiuchumi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Suala la kukithiri kwa PhD mchongo lisifumbiwe macho*

**BUNGE** la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, juzi lilimaliza Mkutano wake wa 10 jijini Dodoma huku mambo mengi yakiwa yamewasilishwa na kutolewa majibu. Miongoni mwa mambo hayo ni taarifa za kamati za kudumu za bunge hilo kuhusu utendaji kazi ambazo ziliibua mambo mazito, kubwa likiwa ubadhirifu wa mabilioni ya shilingi katika halmashauru kadhaa nchini.

Kubwa kuliko yote ni sakata la kuwapo kwa shahada za mchongo za udaktari wa falsafa ambazo hivi sasa zimezagaa kila kona. Hatua hiyo ilisababisha mbunge mmoja kuhoji juu ya uhalali wa shahada hizo ambazo zimesababisha hata wale ambao hawakufika hata kidato cha nne kuitwa madaktari wa falsafa kwa maana kwamba wamezipata shahada hizo za heshima kutokana na mambo waliyoyafanya katika jamii.

Jambo hilo liliwaibua Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolph Mkenda na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ambao ni wasomi wabobezi katika uchumi na sheria na kabla ya kuwa na nyadhifa hizo baada ya kuwa wabunge, waliwahi kufundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Bila kuuma maneno, Prof. Mkenda alisema shahada za PhD zinatolewa katika namna tatu, moja ikiwa ya kusoma darasani kwa kuhudhuria mihadhara na kufanya utafiti na hatimaye kuandika tasnifu kuhusu jambo fulani ambalo mhusika hufika mbele ya jopo la maprofesa na madaktari wa falsafa wabobezi. Wakikubali kuwa amekidhi viwango, basi hupasishwa tayari kutunukiwa shahada hiyo.

Namna ya pili, haitofautiani sana na ile ya kwanza kwani mhusika huchagua mada na kuandika andiko la utafiti na atakapokubaliwa anaweza kuanza na pindi atakapomaliza, hufika mbele ya jopo la wanazuoni kujitetea na hatimaye kutunukiwa shahada. Ya tatu, ni ile ya mtu kupewa shahada ya udaktari wa heshima (Honoris Causa) ambayo mtu hupewa kutokana na mambo aliyoyafanya katika jamii au uongozi.

Katika eneo hilo la tatu, chuo kikuu husika huweka vigezo na kufuatilia kazi alizofanya ama katika uongozi au masuala ya kijamii, hasa katika kutatua changamoto zinazoikabili jamii inayohusika. Iwapo atakidhi vigezo hivyo, chuo hicho humpatia shahada hiyo ya heshima wakati wa mahafali ambayo hujumuisha wanafunzi wengine wanaohitimu kwa mwaka husika.

Pamoja na kuwapo kwa vigezo hivyo, hivi sasa wako watu ambao wamekuwa wakidaiwa kununua shahada hizo kwa kati ya dola za Marekani 1,500 hadi 5,000 kulingana na matakwa ya chuo. Hatua hiyo imesababisha hata ndani ya Bunge kuwapo watu wanaojiita madaktari jambo ambalo limetia ukakasi juu ya uhalali wa sifa hizo.

Kama alivyosema Spika Tulia, ni vyema PhD hizo za mchongo zikachunguzwa kuhusu uhalali wa vyuo hivyo kuwatunukia watu hao badala ya kuibuka kila uchao kuwa mtu fulani anaitwa daktari wa heshima. Baadhi ya wanaoitwa hivyo hawana hata vyeti vya kidato cha nne na wengine walifeli mitihani ya kidacho cha nne.

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, suala la kuwapo kwa madaktari wenye Ph.D za mchongo lilianza kuota mizizi ndani ya bunge na katika jamii lakini likakoma baada ya msomi mmoja kuandika kitabu kilichoitwa 'Mafisadi wa Elimu' kwa kuwachambua wale wote waliodaiwa kuwa madaktari na wengine kuzikana shahada hizo. Lakini sasa jambo hilo limeibuka kwa kasi na kama ilivyokuwa awali, wabunge ndio wanaongoza kuwa na aina hizo za shahada.

Ni vyema kasi hiyo ya kukithiri kwa PhD za mchongo ikadhibitiwa vinginevyo tunaweza kujikuta kila mtu mtaani anaitwa daktari wa heshima ilhali hastahili hata sifa hiyo. Pia vyuo vinavyotoa shahada hizo, vichunguzwe kama vina ithibati inayotambulika kimataifa au ni chuo mradi chuo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# *Upotoshaji huu hatari vita dhidi ya ukeketaji, ungemulikwa haraka*

Na Sabato Kasika

**UKEKETAJI** ni neno ambalo huibua jazba na hisia tofauti kila mara linapotajwa, katika pande mbili, kuanzia kwa watetezi wa mila na utamaduni huo, huku wanaopinga ukatili huo wakitumia njia mbalimbali kuhakikisha unakomeshwa.

Wakati vita dhidi ya ukeketaji ikiendelea, wanaojihusisha na ukatili huo nao wamekuja na elimu mpya wanayoisambaza na kuwatia hofu baadhi ya watu ili iwe rahisi kuruhusu watoto wao kukeketwa.

Elimu ambayo inadaiwa kusambazwa na baadhi ya wale wanaoendekeza mila potofu hizo na kuitia hofu jamii, ni kuwaambia wazazi kwamba, watoto wasipokeketwa, wanaweza kukumbwa na ugonjwa wa fistula.

Kutokana na hofu ya watoto wao kukumbwa na ugonjwa huo, wazazi wanalazimika kuruhusu watoto wao wakeketwe, kitendo ambacho kinaendelea kuwaweka watoto hao katika hatari zaidi ya kiafya.

Hayo yanaibuliwa na Mtandao wa Kupinga Ukeketaji Tanzania, huku mkoa wa Singida ukitajwa kuwa kinara wa elimu hiyo inayowatia hofu wazazi na kulazimika kukeketa watoto wao wachanga kwa kutumia kucha.

Getrude Dyabene, Mratibu wa Mtandao huo, anasema wamefanya utafiti na kubaini kuwapo kwa elimu hiyo mkoani Singida, na kwamba jitihada zaidi zinahitajika kuhakikisha jamii inapata elimu sahihi.

Ni katika kilele cha maadhimisho ya Kupinga Ukeketaji Duniani, Februari 6 mwaka huu, yaliyokuwa na kaulimbiu isemayo; "Wanaume na wanawake tushiriki kupinga mila na desturi zenye madhara, ili kutokomeza ukeketaji".

Anakumbushia takwimu za Wizara ya Afya kuwa mkoa wa Manyara bado ni namba moja ukiwa na asilimia 58 katika ukeketaji, Dodoma asilimia 47, Arusha asilimia 41, Mara asilimia 32 na Singida asilimia 31.

**Hayo yanaibuliwa na Mtandao wa Kupinga Ukeketaji Tanzania, huku mkoa wa Singida ukitajwa kuwa kinara wa elimu hiyo inayowatia hofu wazazi na kulazimika kukeketa watoto wao wachanga kwa kutumia kucha.**

Ni kweli kwamba, pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali na wadau wake, katika kutokomeza vitendo hivyo, ni wazi bado kuna mambo ya kufanya, ili kuondoa mila potofu zinazohatarisha maisha ya watoto wa kike.

Miongoni mwa mambo hayo ni utoaaji wa elimu kuhusu madhara ya ukeketaji na pia kujua chanzo cha fistula, lakini pia jamii iungane ili kukemea ukeketaji na kushirikiana na vyombo vya dola kwa kutoa taarifa na ushahidi.

Njia hiyo inaweza kusaidia jitihada za kupambana na ukeketaji na pia kuiondoa jamii yenyewe katika elimu potofu kwamba kukeketa kunazuia mtoto wa kike asipate ugonjwa wa fistula wakati si kweli.

Kwa mujibu wa wataalam wa afya, ukeketaji una madhara makubwa kwa wanawake na watoto wa kike, ikiwa ni pamoja na hatari wakati wa kujifungua kwa kupoteza damu nyingi pamoja na vifo vya wanawake.

Lakini pia wataalam hao wanaeleza kuwa, kukeketa kunasababisha ugonjwa wa fistula, utasa, ugumba na madhara ya kisaikolojia, hivyo kwa maelezo hayo, ukeketaji kwamba, unapaswa kupingwa kwa nguvu zote.

Dk. Peter Mjinge wa Hospitali ya CCBRT anafafanua kuwa ugonjwa wa fistula ni tundu lisilo la kawaida linalokuwa kati ya njia ya uke na njia ya kibofu cha mkojo na pia linaweza kati ya njia ya uke na njia ya haja kubwa.

Katika mazingira hayo, mgonjwa hutokwa na haja ndogo au kubwa bila hiari yake, na kwamba tatizo hilo, zaidi husababishwa na mtu kupata maumivu au uchungu wa uzazi kwa muda mrefu wa zaidi ya saa 24 wakati wa kujifungua.

Hivyo, kwa maelezo hayo ya wataalam wa afya, ni wazi hakuna uhusiano wowote wa mwanamke au mtoto wa kike asiyekeketwa kupata fistula, bali ni ujanja wa kutaka kuendelea kuhalalisha mila potofu.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Wajua mahakama isipotimiza wajibu wake wananchi wanaweza kuishtaki?



Pascal Mayalla

NAOMBA kuanza safu hii kwa kutoa pongezi na kongole kwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamisi Juma, kwa hotuba yake Siku ya Sheria kwa mwaka huu, iliyosisitiza umuhimu wa usuluhishi katika kutatua migogoro badala ya kukimbilia mahakamani.

Kwa Maslahi ya Taifa, leo inachambua sehemu ya hotuba ya Jaji Mkuu kwenye Siku ya Sheria ya mwaka 2023 iliyofanyika katika uwanja wa Chinangali jijini Dodoma. Kwa vile nawaandikia wananchi wa kawaida kabisa, baadhi ya vifungu vya sheria nitaviacha na kuwaachia wanasheria kwa kuwa wananchi wa kawaida wanachotaka ni haki, kutendewa haki na haki kuonekana inatendeka.

Kaulimbiu ya Siku ya Sheria mwaka huu ilikuwa "UMUHIMU WA UTATUZI WA MIGOGORO KWA NJIA YA USULUHISHI KATIKA KUKUZA UCHUMI ENDELEVU: WAJIBU WA MAHAKAMA NA WADAU." Jaji Mkuu Prof. Juma amesema umuhimu wa usuluhishi katika utatuzi wa migogoro ni kwa mujibu wa Ibara ya 107 ya Katiba inayoitaka Mahakama katika kutoa uamuzi wa mashauri, inatakiwa kuzingatia kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro. Kanuni hii ya Katiba inazingatia faida kubwa za matumizi ya usuluhishi katika utatuzi wa migogoro ikijumuisha kupunguza gharama na muda wa kuendesha shauri na kuendeleza undugu miongoni mwa wadaawa.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeweka kanuni mbili muhimu ambazo bado hazizingatiwi kikamilifu na mhimili wa mahakama wakati wa kusikiliza mashauri mahakamani, hivyo kusababisha ucheleweshaji mkubwa wa mashauri na kuongeza gharama za uendeshaji wa mashauri.

Ibara ya 107A (2) (d) imetamka kanuni inayoitaka Mahakama, wakati inasikiliza mashauri ya madai au jinai, kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro. Ibara ya 107A (2) (e) imetamka kanuni nyingine muhimu sana kuwa katika kutoa uamuzi wa mashauri ya madai na jinai kwa mujibu wa sheria, mahakama zitende haki bila kufungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi yanayoweza kukwamisha haki kutendeka.

Tumeshuhudia wananchi wengi wakikosa haki zao mahakamani kwa kesi kutupwa kwa sababu tu ya kukosea kwenye masharti ya kiufundi ya kisheria (legal technicalities). Mfano mzuri ni kesi ya mwanasiasa Zitto Kabwe alipovuliwa unachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) akiwa Naibu Katibu Mkuu. Kwa mujibu wa Katiba ya CHADEMA, mamlaka ya nidhamu ya Naibu Katibu Mkuu ni Baraza Kuu. Sasa Kamati Kuu ya CHADEMA ilipata wapi uwezo wa kumfuta uanachama wakati si mamlaka yake ya nidhamu? Zitto alikimbilia mahakamani na kesi yake ikatupwa kwa makosa ya kiufundi, hivyo kupoteza haki yake.

Baada ya kushindwa kesi, Katiba ya CHADEMA ikaweka kifungu kinachokwenda kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mwanachama wa CHADEMA haruhusiwi kufungua shauri mahakamani na akifungua, akishindwa anakuwa amejifukuzisha uanachama! Kwa hiyo Zitto baada ya kushindwa kesi, akafungasha kwa kuliaga Bunge na kuwaaga wabunge wenzake huku Chadema wakishangilia kumtimua. Sasa hivi kuna kesi nyingine mahakamani ya mazingira yale yale kama ya kesi ya Zitto. Ni matumaini kwamba safari hii mahakama itatenda haki.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari limetunga sheria kufanikisha matumizi ya usuluhishi kwa kupitisha Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.1 ya mwaka 2020 [Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act No. 1 of 2020] iliyozifanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai (Sura ya 33) kwa kuongeza Kifungu kipya cha 64A, kinachotamka kuwa wadaawa, sasa wana hiari ya kutatua migogoro wao nje ya mahakama.

Iwapo wadaawa watafikia makubaliano nje ya mahakama, watayasajili katika ngazi husika ya mahakama na makubaliano hayo yatakuwa na nguvu ya amri ya mwisho ya mahakama katika mgogoro huo.

Ni wajibu wa majaji, mahakimu, mawakili wa serikali na mawakili wa kujitegemea; kila mara kuwakumbusha wadaawa uwapo wa nafasi hiyo ya kutatua migogoro nje ya mahakama kwa nia hiyo hiyo ya kuwataka wenye migogoro kutumia usuluhishi badala ya kukimbilia mahakamani.

Hii iboreshwe zaidi kwa kutungwa sheria kuwa kesi zote za madai, lazima kwanza zianzie usuluhishi na baada ya kushindwa kuafikiana, ndipo ziende mahakamani.

Jaji Mkuu Prof Juma, ameipongeza Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuweka mazingira ya kisheria ya kusuluhisha migogoro nje ya mahakama kwa kutoa orodha ya wasuluhishi kwamba mihimili ya Bunge na Serikali inatambua usuluhishi ni tiba ya ucheleweshwaji wa mashauri mahakamani. Kaulimbiu hii, inatoa tahadhari kwa majaji, mahakimu, mawakili wa serikali na mawakili wa kujitegemea ambao ndio wahusika wakubwa wa uendeshaji wa mashauri mahakamani. Mihimili ya Bunge na Serikali, tayari imeelewa kuwa dawa ya ucheleweshwaji wa mashauri mahakamani ni usuluhishi ambao tayari umewezeshwa kwa kutungiwa sheria nyingi katika maeneo mbalimbali ambayo usuluhishi unawezekana.

Mhimili wa Mahakama na wadau wake, wataonekana kuwa wameshindwa mtihani wa viapo vyao na wajibu wao kulinda na kutetea Katiba na sheria za nchi wasipotekeleza wajibu wao wa kufanikisha usuluhishi.

Wananchi wanayo haki kuushtaki mhimili wa Mahakama kwa mhimili wa Bunge, wakiona haki inachelewa kwa kujiuliza kwa nini mhimili wa Mahakama hautumii sheria zilizotungwa na Bunge kuwasaidia wananchi kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi?.

Upo ushahidi kuwa mihimili ya Bunge na Serikali ina ufahamu mkubwa kuhusu manufaa ya usuluhishi.

Mhimili wa Mahakama na wadau wake, tukiwamo sisi mawakili, tutajiweka katika mazingira hatari mbele ya macho ya wananchi, endapo hatuzitumii sheria zinazotoa nafasi za usuhishi na sheria zinazotuzuia kutumia kanuni za kiufundi kuchelewesha haki.

Tukutane wiki ijayo kwa muendelezo wa makala hii kuhusu umuhimu wa usuluhishi na jinsi Rais Samia Suluhu anavyotumia suluhu ya usuluhishi kuliponya taifa kwenye mtanzuko wa kisiasa, hivyo kujikuta tunajiponya kiuchumi na kijamii.

**Wasalaam**
**Paskali**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Shahada ya uzamivu si kuangua madafu



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

MIAKA ya zamani, wakati na baada ya muda mfupi wa nchi hii kujipatia uhuru, mtu aliyehitimu darasa la nne alionekana msomi, aliyemaliza darasa la saba msomi kwelikweli wa sekondari we acha tu!

Mtu aliyesoma mpaka Makerere (Uganda) huyo alikuwa hashikiki katika jamii kwa sababu alikuwa wa daraja la juu sana. Ndivyo walivyokuwa watu kina Mwalimu Julius Nyerere ambaye baadaye alikuja kuwa mkuu wa taifa hili.

Jina Makerere lilipata umaarufu sana nchini kutokana na Mwalimu Nyerere kusoma hapo masomo ya chuo kikuu. Kwa msiojua, Makerere ni chuo kikuu cha mwanzo mwanzo katika eneo hili la Afrika Mashariki.

Ndicho chuo walikosoma wakubwa wengi waliokuja baadaye kuongoza mataifa yao. Benjamin Mkapa (Rais wa Awamu ya Tatu wa Tanzania) naye alisoma Makerere lakini hakufikia ngazi ya udaktari wa falsafa, vivyo hivyo kwa Nyerere.

Lakini baadaye Nyerere alikuja kupata udaktari wa heshima mara nyingi tu tena akitambuliwa na vyuo vikuu mbalimbali duniani. Hata hivyo, sikupata hata siku moja tangu nimjue mpaka anafariki dunia mwaka 1999, kumsikia akijiita Dokta Nyerere!

Mtaalamu wa masuala ya uchumi, Profesa Adolf Mkenda ambaye ni Waziri mwenye dhamana ya elimu nchini, anakwambia udaktari una ngazi tatu; wa kusomea darasani, wa kufanya utafiti na wa kugawiwa kwenye kisahani, ukiitwa wa heshima.

Udaktari wa kwanza na pili, unastahili mtu kuitwa Dokta nanihii kwa sababu ya kuusotea kuliko huu wa kupeana mitaani kwa kuwa tu mtu kakufurahia kwa ofa na vituko vyako au kwa kuwa tu umempa fedha, yaani umeununua kama dafu.

Nchi hii tumepata kuwa na madaktari kama vile Dokta Remmy Ongala, Profesa Maji Marefu, Dokta Matunge na wengineo kwa kuitwa tu na watu kutokana na uganga au usanii wao na ndiyo sababu hata waganga wa kienyeji wanajiita Dokta naniliu ili kujiongeza sifa.

Leo tunashuhudia tuna wabunge wanaitwa madokta kwa sababu tu wametunukiwa heshima hizo kwa kununua au kwa kufurahiwa tu na watu kwa mambo yao au misaada yao, nao kufikia hatua ya kujimwambafai kuwa wanaweza kutoa mihadhara vyuo vikuu! Mungu apishie mbali!

Inashangaza kuona hivi sasa kila Mtanzania anataka aitwe dokta! Inawezekana kwa namna hii miaka mingi ijayo, tukajikuta kila mtu ni dokta hata mtoto mdogo kutokana tu na matakwa, lakini na urahisi wa kuupata.

Kama hivi sasa zinaibuka asasi zisizo za kiserikali ughaibuni huko, kufanya biashara ya udaktari wa heshima. Nani atashindwa kuununua ili mradi ajimwambafai kwa jamii yake, hata kama hana mchango unaotukuka?

Tumeyataka wenyewe kwani haishangazi, mathalan kuona leo mwanafunzi wa chekechea anafanya mahafali huku amevalia joho kama la chuo kikuu, bila kujali kuwa joho hilo ni vazi la heshima ya kitaaluma linalotakiwa kuvaliwa na aina fulani ya watu.

Leo mtu anahitimu darasa la saba au la 12 anavalia joho kama mhitimu wa chuo kikuu na tunanyamaza tu! Lakini sasa watu wamekubuhu na kununua shahada za uzamivu na kuziita za heshima, ndo tunaibuka kizani na kulalamika. Tuwaache tumeyataka.

Ni mazoea tu, dereva wa basi anajiita rubani kana kwamba anaendesha ndege, tunacheka tu na kumpongeza. Tuna marais wa kila kitu hivi sasa, rais wa chama, rais wa soka, rais wa mieleka, rais wa ndondi na kadhalika, mbona hatulii?

Tukitaka tusiumizwe na kina Dk. Musukuma, Dk. Taletale, Dk. Abood, Dk. Sophia, Dk. Ritha, Dk. Jesca na madokta wengine, ni kuchukulia tu kuwa hiyo ni misimu na itatoweka na hata tunapotaka kuwatambulisha tuache kutaja udokta wao, tuwaachie wao na familia zao kutambuana.

Haiwezekani Profesa Kitila Mkumbo asotee udokta kwa miaka nenda rudi, akiwasilisha tasnifu zake kedekede kwa vigogo wengine wa elimu duniani na hatimaye atunukiwe na kufanya utafiti mbalimbali wa kitaaluma pamoja na kuchapisha katika majarida mbalimbali duniani, leo aje mtu na ukwasi wake anunue udaktari na watambulishwe sawa! Hapana!

Tuache kushusha hadhi ya udaktari kirahisi hivi kwani tutawavunja moyo wale wanaosimamia wasomi wa shahada hizo za uzamivu na kuonekana kuwa hawana walifanyalo bali kupoteza muda kwani hivi sasa kuna madalali wa shahada hizo na ukizitaka ni misuli yako tu ya kiuchumi! TCU fumbueni macho tulikatae hili. **Alamsiki!**

## Madiwani kupewa vishikwambi

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

HALMASHAURI ya Itigi wilayani Manyoni mkoani Singida imepanga kuwanunulia vishikwambi madiwani na watalaamu kwenye ofisi ya mkurugenzi kwa mwaka wa fedha wa 2023/24.

Mkuu wa Divisheni ya Mipango, Emmanuel Dyelu, akizungumza juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo, alisema halmashauri imeomba kuidhinishiwa Sh. bilioni 8.1 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Dyelu alisema vipaumbele vya bajeti hiyo ni pamoja na ununuzi wa vishikwambi kwa ajili ya madiwani na wataalamu kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, kutekeleza mpango wa kutenga asilimia 10 kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Vipaumbele vingine ni kuboresha miundombinu ya elimu na afya pamoja na kuandaa mpango kabambe wa halmashauri ili kwenda na kasi ya ukuaji wa mji.

Katika kikao hicho, madiwani walipitisha randama ya bajeti ya zaidi ya Sh. bilioni 26.9 kwa mwaka 2023/24 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za halmashauri.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, Hussein Simba alisema halmashauri hiyo imeendelea kufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Simba aliwataka madiwani hao kusimamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye maeneo yao na kuishukuru serikali kwa jinsi ambayo imeendelea kupeleka fedha za kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika halmashauri hiyo.

Diwani wa Itigi Mjini, Ali Minja akichangia mjadala huo, alisema halmashauri inapaswa kutenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara mpya kwenye maeneo yasiyo na miundombinu hiyo ili kuongeza thamani ya maeneo na viwanja vinavyouzwa na halmashauri.



Mkurugenzi wa Shafa Agro, Mohammed Nasser akizungumza wakati wa semina ya kuitambulisha kampuni mpya ya ufugaji na uuzaji vyakula vya mifugo ya Shafa Mills kwa wadau wa Sekta ya ufugaji, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

### KAMATI YA BUNGE:

# Wananchi wote walioathiriwa tope la mgodi walipwe fidia

**Na Romana Mallya,** DODOMA

MKUTANO wa 10 wa Bunge la 12 uliahirishwa juzi jijini Dodoma huku moja ya maazimio ya chombo hicho ni wananchi wote walioathiriwa na tope baada ya kupasuka kwa Bwawa la Mgodi wa Almasi wa Williamson Diamond Ltd, walipwe fidia inayoendana na thamani ya mali zao kwa sasa.

Ajali hiyo ilitokea Novemba 7 mwaka jana na kusababisha hasara kubwa kwa wananchi baada ya tope hilo kufunika nyumba na mashamba yao.

Akisoma bungeni taarifa ya mwaka ya shughuli za kamati, Makamu Mwenyekiti wa KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Seif Gulamani alisema ni muhimu tathmini ifanywe haraka ili wananchi hao walipwe fidia na watu wote waliosababisha uzembe wawajibishwe.

"Ni rai ya kamati kuwa ili kudhibiti matukio ya kupasuka kwa mabwawa ni vyema kukafanyika ukaguzi wa mara kwa mara kwenye migodi na maeneo ya uchimbaji ili kubaini upungufu mbalimbali na kuelekeza migodi husika kurekebisha upungufu huo," alisema.

Gulamani alisema kamati inaona kwamba ili kuyadhibiti mabwawa kupasuka, ni vyema kukafanyika ukaguzi wa mara kwa mara kwenye migodi na maeneo ya uchimbaji.

"Pamoja na maelezo yaliyotolewa kuhusu sababu za kupasuka kwa bwawa hilo, kamati imebaini kuwa mgodi ulishindwa kuchukua hatua madhubuti na kwa wakati ili kudhibiti hatari hiyo.

"Pia tumebaini kukosekana kwa huduma ya maji kwa matumizi ya nyumbani kwa wananchi waliopo vijiji vya jirani kutokana na bwawa la maji la New Almasi linalotumika kwa matumizi hayo kujaa tope kutoka kwenye bwawa lililopasuka.

"Uchafuzi wa mazingira yaliyo ndani ya leseni ya mgodi; kufungwa kwa baadhi ya njia zinazounganisha eneo moja na lingine zilizokuwa zinatumiwa na wananchi; na kusimama kwa uzalishaji wa mgodi na hivyo kusababisha kukosekana kwa mapato kwa kampuni na serikali," alisema.

### HALI YA UMEME

Gulamani pia alisema kamati hairidhishwi na hali ya upatikanaji wa umeme nchini huku kukiwa na ucheleweshwaji wa kukamilika kwa baadhi ya miradi.

"Kuanzia mwezi Agosti 2022, maeneo mengi ya nchi yamekuwa katika mgawo wa umeme. Wizara imekuwa ikieleza changamoto mbalimbali kama vile ukame ambao umesababisha vyanzo vya kuzalisha umeme kwa kutumia maji kutotumika kwa uwezo wake wa juu.

"Pia uhaba wa gesi asilia ya kutosha inayoweza kuendesha mitambo ya gesi asili ambayo ipo katika uzalishaji; na uchakavu wa miundombinu ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme," Gulamali alibainisha.

Alisema kamati inaona serikali ina kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha kunakuwa na umeme wa kutosha nchini.

"Serikali inapaswa kuchukua jihada za makusudi hususan kutumia gesi asilia na kuhamasisha uzalishaji wa umeme wa nishati jadidifu ili kuongeza uzalishaji wa umeme nchini. Athari za kuchumi zitokanazo na kukatika kwa umeme ni kubwa sana," alihadharisha.

### BOMBA LA MAFUTA

Gulamani pia alisema pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Chongoleani (Tanga) kufikia hatua mbalimbali ikiwamo ulipaji fidia, kamati imebaini kuwapo changamoto ya pingamizi la mradi kutoka kwa wanaharakati wa mazingira na kuishauri serikali iendelee kutoa ufafanuzi dhidi ya taarifa kinzani.

Kuhusu utekelezaji wa miradi ya madini yenye ubia baina ya serikali na sekta binafsi, Gulamali alisema pamoja na hatua mbalimbali kamati imebaini baadhi ya mikataba ya kikodi kutokamilika kwa wakati na kuchelewa kuhuisha taarifa za upembuzi yakinifu (feasibility study) kwa baadhi ya miradi kulingana na hali halisi ya sasa.

Waziri wa Nishati, January Makamba alisema wanafahamu changamoto ya kukatika umeme bado ipo, akisisitiza kuwa wanayo mipango madhubuti ya kuifumua gridi nzima ya taifa na kuirekebisha kwa kuwa tatizo kubwa ni uchakavu wa miundombinu.

Pia alisema serikali imeweka utaratibu mpya wa kutafuta makandarasi wa ujenzi wa miradi ya umeme ikiwamo katika Wakala wa Nishati Vijijini na Mijini (REA) ambapo miongoni mwa vigezo ni kutowapa zabuni wale wenye malimbikizo ya miradi.

# MAISHA

FEBRUARI 12, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14


## Kashata nazi, maziwa

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

Panga ratiba ya kusafisha nyumbani kwako




## KATUNIKA

Ukurasa 16



# HARUSI

Ukurasa 12


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | 8 | 7 | 3 | 5 | 6 | 3 | 7 | 1 | 7 | 3 |
| 8 | 1 | 3 | 8 | 6 | 8 | 5 | 8 | 2 | 6 | 4 |
| 8 | 3 | 7 | 8 | 3 | 9 | 7 | 5 | 8 | 8 | 7 |
| 1 | 9 | 4 | 7 | 6 | 7 | 8 | 9 | 5 | 7 | 8 |
| 1 | 9 | 0 | 4 | 8 | 6 | 7 | 3 | 9 | 5 | 7 |
| 4 | 5 | 6 | 9 | 0 | 4 | 8 | 9 | 8 | 4 | 7 |
| 9 | 9 | 5 | 8 | 7 | 9 | 5 | 7 | 5 | 9 | 5 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Z | U | A | ■ | K | W | A |
| A | ■ | U | F | A | ■ | T |
| M | ■ | ■ | ■ | T | ■ | W |
| B | E | I | ■ | A | M | A |
| E | ■ | N | ■ | ■ | ■ | N |
| Z | ■ | Z | N | Z | ■ | G |
| I | N | I | ■ | A | Y | A |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

PUA, TAI, ODO, SAA, SU, BA, ITA, GIA, ANGAZIA, JAMBO, SUKIA, TANGAZO

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

SHUHUDIA jinsi mgambo walipokwenda kumkamata jamaa mmoja

**Mgambo:** Hodi, hodi
**Jamaa:** Kimya
**Mgambo:** Hodi, hodi wenye nyumbaa
**Jamaa:** We nani kwani?
**Mgambo:** Sisi mgambo
**Jamaa:** Sawa, mnataka nini?
**Mgambo:** Kuongea na wewe
**Jamaa:** Kuongea na mimi?!
**Mgambo:** Ndio
**Jamaa:** Mko wangapi?
**Mgambo:** Watatu
**Jamaa:** Kama mko watatu si muongee wenyewe...!!!

**SWALI**
Paka ana manufaa gani kwa binadamu?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Bora ndoa ife nipone kipigo!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu za maisha Ndivyo Yalivyo. Bado tuko kwenye anga la ndoa na uhusiano. Hili ni eneo muhimu sana kwani ndio chimbuko la familia zetu.

Pamoja na ukweli kwamba ndoa ni baraka toka kwa Mungu, nyingi zimekuwa shubiri. Wanandoa wengi wako mahakamani kudai talaka baada ya maisha kuwa tofauti na walivyotarajia. Walisahau kuwa ndoa ni mchakato na changamoto ni sehemu yake!

Ndoa nyingi zimegubikwa na wivu, ulevi, ushirikina, uasherati, maagano, laana, mizimu na zaidi ya yote kutokumcha Mungu muumba na mlinzi wa vyote!

Mama mmoja akatoa ushuhuda jinsi alivyotaabika kwenye ndoa yake. Akasema tokea aishi ndani ya ndoa miaka mitatu na kujaliwa kuzaa mtoto mmoja, hajafurahia maisha aliyotarajia. Ni maumivu kila iitwapo leo.

“Mume nilimpenda sana lakini sijui kwa nini alibadilika ghafla na kugeuka bondia kwa kunipiga kila wakati. Nikachoka na kufungua shauri la talaka mahakamani, nikaona bora ndoa ife nipone kipigo cha ‘mbwa mwizi’. Kila niliyemwomba ushauri, wakiwamo wazazi wangu, waliniambia toka asije kukutoa roho. Shauri lilisikilizwa, ndoa ikavunjika leo niko huru!

Msomaji wangu, huo ni mfano mmoja tu. Wako wengi wanateseka kwenye ndoa, wanavumilia au hawajui wapeleke wapi kilio chao. Wakati mwingine unaweza kudhani tatizo ni mwanamume kumbe ni mwanamke mwenyewe.

Swali kubwa hapo ni je, ndoa zetu zimejengwa katika misingi gani? Hebu leo nikutajie hatua kadhaa zinazopaswa kuchukuliwa na wenye haki ili kuondokana na misingi mibaya katika ndoa zao.

Jambo la kwanza ni muhimu kurudi katika misingi ya kule ulikotoka. Jiulize, nimetoka katika familia yenye misingi ipi? Je, ni mambo yapi yanaweza kuniletea matatizo katika ndoa yangu?

Je, ni mambo gani wazazi wangu walifanya aidha kwa kufahamu au kwa kutofahamu ambayo yanaweza kuathiri ndoa yangu? Je, ninafuatiwa na kifungo au laana ya aina gani? Je, kuna mambo gani ya siri ambayo yanaweza kusababisha matatizo katika ndoa yangu?

Jambo lingine la kujiuliza ni je, hii ndoa yangu ninaijenga katika misingi mibovu? Je, kuna mbegu mbaya niliyoipanda inayoweza kuharibu ndoa yangu? Ni lazima ujibu maswali haya mwenyewe.

Kumbuka huwezi kuendelea vyema katika ndoa yako kama hujachunguza misingi yako. Ni muhimu uchukue muda wa kutosha kutafakari suala hili. Pia ni lazima uwe tayari kupambana na nguvu zozote za kishetani zinazoshikilia ndoa yako.

Jambo lingine unalopaswa kulichukulia hatua kwa uzito mkubwa ni kutubu na kuungama makosa yako. Watu wengi dhambi zimewafarakanisha na uso wa Mungu. Mungu hawezi kulinda ndoa yako kama umejificha kwenye kichaka cha dhambi.

Ni lazima utubu dhambi zako zote kwa kudhamiria kuziacha. Unapoungama na kutubu, utahamishwa kutoka katika misingi mibovu ya ndoa na kupewa ushindi mkubwa, na hivyo kupata mafanikio makubwa katika ndoa yako!

Ungama dhambi zako na umwahidi Mungu kuwa hutarudia kutenda uovu. Kama utaficha dhambi zako, shetani ataendelea kuzitumia kama silaha kuitesa ndoa yako. Tubu leo na kupata mabadiliko makubwa sana katika ndoa yako.

Pia unapaswa kufanya maombi makali ya vita. Msingi imara wa maisha yako unapatikana pale tu unapofanya maombi makali ya vita. Wako wanaume au wanawake hawatakaa waoe au kuolewa mpaka pale watakapomwomba Mungu kwa kudhamiria. Huo ndio ukweli.

Shetani anajua akikukubalia kufanikiwa katika eneo hili la ndoa, atapoteza mambo mengi sana. Ndio maana watu wengi sana wamepambana katika eneo hili. Fanya maombi ya vita na kufunga kwa kudhamiria, Mungu atakujibu.

Hatua nyingine ni kuvunja maagano yaliyoasisiwa na viongozi wa koo zetu tokea asili. Mengine tumeyaweka wenyewe, ikiwamo kwa waganga. Ndoa yako inaweza kuwa na matunda, ushindi, maendeleo na nuru kama ukivunja maagano.

Ukiingia kwenye ndoa na bado maagano ya kuzimu, mizimu na wachawi vinakufuatilia, hautafanikiwa katika ndoa yako. Pia fanya maombi ya kuvunja laana za vizazi zinazokufuatilia. Ndoa iliyojengwa katika misingi ya laana itakuwa kama jehenamu ya moto duniani.

Kingine jichunguze mara kwa mara kujirejesha upya Ni ili shetani asipate nafasi kuingilia ndoa yako.

***Naamini msomaji umejifunza kitu hapo. Una kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# PhD za mchongo, dhana nyingine ya udumavu

DHANA na nia njema vimewagharimu watu sana katika maisha. Makosa mengi hufanywa kwa kuendekeza dhana. Hizi kelele zinazoendelea kuhusu mchongo wa digrii ya heshima (Honorary Doctorate-PhD au Honoris Causa) ni zao la kupenda kudhani.

Mtu anadhani kwamba akipata digrii ya heshima katika utu, atakuwa amejitengenezea pepo yake ya mafanikio na heshima duniani, kumbe anatengeneza kizazi cha watu ambao ni wavivu wa kufikiri, kutafiti na kuja na mrejesho wa kitaaluma, wenye tija na maslahi mapana kwa jamii inayomzunguka na taifa kwa ujumla.

Katika nchi yetu na duniani kwa ujumla, wako watu wanastahili na walistahili kupata heshima hiyo ya kutunukiwa digrii za heshima kutokana na michango yao katika jamii na taifa, uchumi, masuala ya kijamii na hata kwa wale walioweka alama katika uongozi uliotukuka.

Wako waheshimiwa wanaotoa ushuhuda kwamba wamepokea ‘ofa’ kutoka vyuo vikuu mbalimbali vya nje kwamba kama wanataka kupata digrii ya heshima, watakiwa kulipia Dola 2,500 hadi Dola 1,500 ili wapewe PhD hiyo. Tunahitaji kufikiri zaidi, kwamba dhana ya kuwa na digrii hiyo ni ili iweje, ili nini?

Februari 9, mwaka huu, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alinukuliwa na vyombo vya habari Bungeni, jijini Dodoma, akisema taifa linahitaji kufahamu utaratibu wa kwenda nao kuhusu PhD za heshima.

Alisema: “Haiwezekani vyuo vya nje vitumwagie digrii za malipo lakini vyuo vikuu vya hapa havioni mchango wenu. Ni muhimu sana sisi kama viongozi na sisi kama taifa kuweka mwongozo mzuri kwa ajili ya wanaotufuata nyuma.”

Kauli ya Spika, Dk. Tulia, ilitokana na mwongozo ulioombwa Bungeni na Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi, aliyetaka kujua kuhusu shahada za heshima zilizotolewa kwa wabunge.

Alitaka kufahamu kwa kiasi gani vyuo hivyo vinavyotoa shahada hizo, vinatambulika na mamlaka za Tanzania zinazosimamia elimu. Alitaka kujua ni vigezo gani vinavyotumika kutoa shahada hizo na ni kwa kiasi gani serikali ya Tanzania inazitambua.

Kama ni kweli serikali huwa inafuatilia uhalali wa chuo kilichomtunuku mtu shahada ya heshima, kufanya uhakiki na kujiridhisha juu ya digrii hiyo, ziko wapi taarifa za uchambuzi wa PhD hizo za mchongo?

Ukweli unauma! Lakini itabaki kuwa kweli kwamba biashara ya PhD za heshima, inadharau mchakato mgumu wenye taabu nyingi, ambazo mtu anapitia kabla ya kustahili heshima ya kutambulishwa kama daktari wa falsafa, mwenye PhD.

Inatia hasira, hasa unapowaona wafanyabiashara wa shahada za heshima walivyobadili heshima hii kuwa zawadi ya dhana huku wakiwaaminisha wale wanaozitafuta kwamba wana nafasi (status) sawa ya heshima na wale waliohenyea PhD zao darasani tena kwa uchache miaka mitatu baada ya kujiunga na vyuo kutokana na sifa zinazokubalika, mojawapo ikiwa shahada ya uzamili au umahiri (masters).

Ni umasikini tu wa fikra, kuwabebesha kwa makusudi heshima itokanayo na kazi ngumu ya kitaaluma kwa watu wasiostahili. Biashara hii ya PhD ya heshima, imeharamishwa zaidi kwa kuacha misingi ya mchakato wa utoaji wa shahada hizi kwa watu wenye michango inayotambulika katika jamii au taaluma husika.

Inakera zaidi pale wachuuzi hawa wa shahada za PhD za heshima na wahitaji wao, wanapoamua kujitambulisha kwa heshima ya udaktari (kwa maana kwamba nao wana PhD. Wengi wao hawajui utafiti ni kitu gani. Hawajui kuna kipengele kigumu cha kwenda kusimama na kuitetea shahada ya uzamivu unayoitafuta mbele ya jopo la wanazuoni wabobezi na wengine hawajui namna inavyotesa wakati wa kukusanya taarifa wakati wa kufanya utafiti juu ya jambo ambalo analifanyia kazi ili kuandika tasnifu ambayo itamwezesha kupata PhD.

Mtu aliyepitia mchakato wa kutafuta elimu kuanzia shahada ya kwanza hadi ya uzamivu (PhD), ana kila sababu ya kufurahia matunda ya kazi nzito aliyoifanya na matatizo aliyopitia hadi kupata ushindi mbele ya jopo la wanazuoni nguli wa upimaji wa kitaaluma.

Waliopata PhD wanajua kwamba kuhitimu kwao si mwisho, bali wana safari ndefu na ngumu ya kukuza ubobezi wao kwa kusoma, kuandika na kuchapisha utafiti wao katika vitabu na majarida mbalimbali ya kimataifa ili kusambaza maarifa na ujuzi wao.

Tuache kuchakachua elimu kwa kila mtu kutaka kuitwa daktari wa falsafa kisa tu kuwa na heshima katika jamii badala ya kuzifanyia kazi.


Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini

***Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

***Simu ya mkononi: +255 767 535490***

HARUSI













## Lusivya na Warda

Januari 27, mwaka huu ilikuwa siku ya kipekee kwa Lusivya Mleh baada ya kufunga ndoa na Warda Hamduni katika msikiti wa Maamur na kisha kufanyiwa sherehe ya kuwapongeza katika ukumbi wa Seabreez jijini Dar es Salaam.

## MITINDO

# WALIOVUTIA GRAMMY 2023

ZULIA jekundu la tuzo za Grammy, linapambwa na mavazi nadhifu ya wasanii ambao huleta ladha tofauti na mvuto wa kipekee.

Mitindo mingi inatambulika hapo kwa mara ya kwanza au inapoboreshwa na kuifanya sherehe nzima kuwa na ushindani mkubwa wa kuvaa.

Mwaka 2023 katika sherehe za utoaji tuzo za Grammy, Cardi B alivutia zaidi kwa kuvalia gauni la Gaurav Gupta ambalo lilianza kuonyeshwa kwa mara ya kwanza kwenye maonyesho ya Couture huko Paris wiki iliyopita.

Anitta aliingia kwenye kumbukumbu ya mavazi kwa kuvaa gauni la Versace ambalo limetoka kwa mara ya kwanza mwaka huu.

Msanii Na Doja Cat alionyesha umaridadi wake kwa kuvalia gauni la Versace lililowekwa pamoja na begi la glasi la Coperni, lilivunja rekodi kwa kuonekana kihalisi.







UREMBO

Na Mary Geofrey



# JINOGESHE KIASILI

KILA mwanamke mwenye haiba ya kike anatamani kuwa mrembo na kuonekana mwenye mvuto kwa watu wanaomtizama.

Urembo wa asili ni salama zaidi kwa kila mwanamke ili udumu na usichuje.

Kupitia safu hii, tutakumbushana mambo muhimu ya kuzingatia ili kuendelea kudumisha urembo wa mwanamke.

**'Moisturize' Daima**

Mwanamke ambaye anajua thamani ya urembo wake ana fahamu umuhimu wa kulainisha ngozi yake.

Ifanye kuwa tabia yako mpya baada ya kutoka ku oga upake moisturizer yako.

Ukitumia mafuta haya uwe na uhakika ngozi yako itakuwa laini, ya asili na yenye mvuto wakati wote bila kuchuja.

Kulala muda wa kutosha

Mara tu unapojua kuwa una siku au tukio kubwa linalokaribia, ratibu usingizi wa mrembo wako.

Kila binadamu anatakiwa kutumia saa 8 kila siku kwa ajili ya kupumzisha mwili wake, sasa ukilala muda pungufu kwa muda mrefu ngozi yako itachuja na kukosa mvuto.

Kulala kwa muda mrefu kunafanya ngozi inang'aa, nywele zinapata afya, kuonekana bora na kila kinachotegemea usingizi kinastawi kwenye mwili wako.

**Ng'oa nyusi zako**

Ikiwa unataka kuhakikisha kuwa unaonekana mrembo kiasili basi hakikisha unang'oa nyusi zako mara kwa mara.

Kuwa na nyusi kamili kutakufanya uso wako wote uonekane mzuri na kundoa zile ambazo zimechoka na wakati mwingine kuingia hadi machoni.

**Itaendelea.....**



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Kashata nazi, maziwa

KASHATA ni kichangamsha kinywa ambacho watu wengi wanapenda kukitumia hasa wanaotumia kahawa kwa sababu wanashushia.

Katika safu yetu leo tutaelekezana namna ya kutengeneza kashata za maziwa ambazo unaweza kula nyumbani na familia yako.

**Mahitaji**

Sukari kikombe kimoja, nazi kikombe kimoja, mdalasini wa kusaga nusu kijiko cha chai, cardamon nusu kijiko cha chai, maziwa vijiko viwili vya chakula, unga wa ngano na rangi (siyo lazima).

**Namna ya kutengeneza**

Pasua nazi, toa ile nyama ya ndani weka kwenye blender, weka na maziwa saga mpaka iwe laini sana. Au unaweza kukuna kwa kutumia kibao cha mbuzi.

Washa moto, bandika sufuria jikoni likipata moto weka sukari, koroga mara kwa mara mpaka iyeyuke na kua brown.

Punguza moto, weka nazi, mdalasini, cardamon, rangi, unga koroga vizuri kwa dakika mbili ili mchanganyiko uchanganyikane.

Chukua sinia lipake mafuta, toa mchanganyiko ule jikoni umwage kwenye sinia chukua kijiko, usambaze uenee vizuri.

**Uache upoe kwa muda.**

Kata saizi unayotaka ukiwa bado wa moto, ukimaliza uache upoe kisha jirambe kwa nafasi.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Panga ratiba ya kusafisha nyumbani kwako

UCHAFU unachangia kwa kiwango kikubwa kuharibu nyumba hata kama ni nzuri na iliyojengwa katika uimara kiasi gani.

Mwingine anaweza kusema mbona kusafisha nyumba ni jambo linaloeleweka, lakini ninachotaka kueleza ni kwa namna gani unatakiwa kuweka kipaumbele na kujiwekea ratiba nzuri ya usafi wa nyumba yako.

Kumbuka kwamba nyumba ikisafishwa kwa umakini na ufasaha ni dawa inayojitosheleza katika kuiimarisha na ikadumu zaidi. Kinyume chake, isiposafishwa vizuri kuna uwezekano mkubwa wa kuharibika na kupoteza mvuto na uimara wake.

Jambo la msingi na la kuzingatia ni kwamba nyumba ina maeneo mengi na kila eneo linahitaji kusafishwa kwa umakini kwa ajili ya ustawi wake.

Ili ufanikiwe katika hilo, ni lazima kujiwekea utaratibu mzuri wa kujipangia ratiba ya namna gani bora ya kufanya usafi katika kila eneo la nyumba yako.

Kwa mfano kama ni jikoni, chumbani, sebuleni, jikoni, nje ya nyumba, stoo, vyooni na katika viunga vyote vya nyumba hakikisha kwamba kote kunafanyiwa usafi wa uhakika kila mara.


Kwenye maeneo yote ya wazi, yakiwamo yale yanayohitaji kufagiwa, hakikisha unafanya hivyo. Kama umepanda maua, yahudumie vizuri kwa kuyawekea mbolea na kuyamwagilia maji pamoja na kuyatengenezea mazingira ya kuendelea kustawi zaidi na yasigeuke kuwa uchafu kwenye nyumba.

Ukimaliza kufanya usafi, hakikisha unakagua kila eneo la nyumba ili kujiridhisha kama endapo kila mahali kumeguswa na usafi na kama kuna vitu ambavyo havihitajiki au havitumiki, viondoe.

Baada ya kusafisha hakikisha kila kitu kwenye nyumba kimepangiliwa inavyostahili kuanzia jikoni, sebuleni, vyumba vya kulala, vyooni na hata nje ya nyumba kwenye bustani na sehemu nyinginezo.

Hakikisha yale maeneo yote ambayo yanahitaji kufanyiwa usafi kila siku inafanyika hivyo na usafi kwenye kila eneo la nyumba yako ndio utaiimarisha lakini endapo hakutakuwa na mpango mzuri wa kuisafisha utaiharibu.





# Jinsi ya kutumia kioo kubadili mwonekano wa ndani

Na Restuta James

Katika mwendelezo wa makala za mapambo ya ndani, leo tunakuletea maajabu ya pambo la kioo na nguvu yake katika kubadili mwonekano wa ndani.

Wataalam wanaeleza kuwa kioo ni pambo ambalo limetumika kwa karne kadhaa na halichuji.

Inaelezwa kuwa kioo kikitumika kupamba chumba kidogo kinabadili mwonekano na kuwa 'kikubwa' na chenye mvuto.

Eneo likiwa kubwa, kioo kinaweza kulibadili na mtu akaliona la kawaida na lenye kuvutia hata kama uhalisia hauko hivyo.

**DONDOO**

1: Jambo la kwanza la kuzingatia unapotaka kutumia kioo kama pambo ni ukubwa wa chumba na wa kioo pia. Mathalani, usitundike kioo kikubwa sebuleni kuliko sofa ambalo liko kwenye ukuta husika wala kisiwe kidogo kuliko nusu ya sofa hilo.


2:Katika eneo la sofa, urefu wa kioo sio tatizo sana bali upana na kinatakiwa kuwekwa nchi sita toka linapoishia sofa lako.

3: Vioo vidogo vina vionjo vyake kama vikiwekwa vingi sehemu moja. Muhimu zaidi ni kupima kile kitakachokuwa kinaonekana kwenye kioo muda mwingi. Wengine hupenda kuweka ua au picha itakayoonekana zaidi kwenye kioo.

3: Jambo lingine unalopaswa kuzingatia ni eneo lenye mwanga. Inaelezwa kwamba kioo kinachotumika kama pambo kikiwekwa karibu na dirisha kinaongeza nuru ndani hivyo kuongeza umaridadi hasa katika chumba kidogo.

4: Eneo la kona linatajwa kufaa sana kuwekwa pambo la kioo kwani kitaonesha ukuta mwingine na mgeni anaweza kudhani ukuta unaendelea na hivyo kuongeza mvuto. Kona ikiwa inatazama mlango inanoga zaidi.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...KWENYE NDOA ZENU KUNA WATOTO WAO...

# Waliokufa kwa tetemeko wafikia 24,000

**INSTANBUL,** UTURUKI

IDADI ya watu waliofariki dunia kutokana na tetemeko la ardhi lililozikumba Uturuki na Syria, imefikia 24,000.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AFP, kati ya hao, 20,665 ni kutoka Uturuki na 3,553 wa Syria, kulingana na takwimu za shirika la habari la AFP.

Licha ya watu hapo kupoteza maisha kutokana na tetemeko hilo lililotokea mapema wiki hii, imeelezwa kuwa mamilioni ya watu hawana makazi na mahitaji ya kibinadamu baada ya majengo kuporomoka na mali nyingi vikiwamo vyakula, kuharibika.

Pamoja na kuelezwa idadi hiyo, vikosi vya uokoaji vya mataifa hayo na vile vya kutoka nje, vimeendelea na kazi hiyo ili kuona kama kuna uwezekano wa kupata watu zaidi waliopoteza maisha na wengine ambao wanaweza kuwa bado hai.

Kuhusu misaada ya kibinadamu, ofisi ya Umoja wa Mataifa ya masuala ya kibinadamu, ilikaririwa na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) kuwa kumekuwa na ugumu wa kuyafikia maeneo yanayodhibitiwa na waasi.

Taarifa hiyo ilisema mpaka jana ni misafara miwili tu ya misaada iliyofika katika maeneo hayo nchini Syria, hivyo kutoa wito wa kusitishwa mara moja kwa mapigano ili kuruhusu msaada kumfikia kila mtu.

**MIUJIZA YAIBUKA**

Wakati hali ikiendelea hivyo, miujiza zaidi imeripotiwa baada ya picha za video zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii kuonyesha mjamzito na bintiye mdogo wakitolewa nje ya jengo lililoanguka katika mji wa Gaziantep, Uturuki baada ya kunusurika kwa saa 115.

Pia kumekuwa na ripoti za watu kadhaa kuokolewa katika maeneo yaliyokumbwa na tetemeko nchini Uturuki baada ya saa 110, akiwemo kijana mmoja.

Habari zaidi zilieleza kuwa juzi, zikiwa siku tano tangu tetemeko la ardhi lilipotokea Uturuki Jumatatu wiki hii, katika mji wa Hatay, mvulana mwenye umri wa miaka 13 aripotiwa kuokolewa kwenye vifusi baada ya kukaa kwa saa 128 kwenye vifusi.

Picha zilionyesha mvulana huyo, Arda Can Ovun, akitolewa nje ya jengo lililoporomoka juzi asubuhi huku juhudi za uokoaji zikiendelea katika eneo la kusini mwa Uturuki lililoharibiwa na tetemeko la ardhi.

**BBC.**



Waokoaji wakiendelea na shughuli za kutafuta watu waliokumbwa na tetemeko nchini Uturuki. **PICHA: MTANDAO.**

# Ugonjwa usiojulikana waua 20

**MALABO,** EQUATORIAL GUINEA

UGONJWA ambao haujajulikana umeibuka katika jimbo la kaskazini la Equatorial Guinea, Kie-Ntem, na kusababisha vifo vya watu 20.

Vifo hivyo vimethibitishwa na mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Olamze, mji ambao uko kilomita chache kutoka mpaka wa Cameroon.

Kwa mujibu wa mamlaka za afya za afya za Cameroon, waliopatwa na ugonjwa huo walikutwa na dalili za kukosa nguvu, kutokwa damu puani, kutapika damu, homa kali na kuharisha.

Taarifa zaidi zilisema juzi kuwa waliokumbwa na ugonjwa na vifo hivyo wanatoka katika maeneo matatu ya kaskazini mwa Equatorial Guinea na kwamba watu wanne kati ya hao wanatoka katika familia moja.

Wataalamu wa afya walibainisha kuwa maradhi hayo yanatokana na mtu kugusana na aliyeambukizwa. Mamlaka za Cameroon zimewataka wananchi kuchukua tahadhari ikiwamo kutokushikana mikono.

Kutokana na ugonjwa huo na vifo vilivyotokea, mamlaka za Equatorial Guinea zimesema Kie-Ntem itakuwa chini ya karantini hadi hapo chanzo cha ugonjwa huo kitakapojulikana.

**BBC**

# Marekani yatungua kitu cha ajabu

**NEWYORK,** MAREKANI

MAREKANI imetungua kitu kisichojulikana ambacho kilikuwa katika anga lake eneo la Alaska. Kitu hicho ambacho kilionekana juzi, kwa mujibu wa Ikulu ya White House, Rais Joe Biden aliamuru ndege ya kivita itungue.

Msemaji wa White House, John Kirby, alisema kitu kisichokuwa na rubani na ukubwa wa gari dogo kilikuwa tishio kwa usafiri wa anga wa raia.


"Madhumuni ya kitu hicho na asili yake haikuwa wazi, ndiyo maana baada ya uchunguzi, amri ilitolewa kitunguliwe," alisema Kirby na hatua hiyo imejiri ikiwa ni wiki moja baada ya jeshi la Marekani kuharibu puto la China juu ya maji ya anga la Marekani.

Akizungumza akiwa Ikulu ya White House juzi, Kirby alisema kitu hicho kilichodunguliwa juzi, kilikuwa na uchafu mdogo ikilinganishwa na puto lililorushwa Jumamosi iliyopita kwenye pwani ya Carolina Kusini.

Kwa mujibu wa Kirby, kitu hicho kilikuwa futi 40,000 (sawa na mita 12,000) na kilionekana kikiwa katika anga juu ya pwani ya anga la kaskazini ya Alaska na kwamba kilikuwa tayari kimevuka Alaska kwa kasi ya kilomita 64 kwa saa na kilikuwa kando ya bahari kikisafiri usawa wa ncha ya Kaskazini kilipotunguliwa.

Baada ya chombo hicho kutunguliwa, helikopta na ndege za usafiri zimetumwa kukusanya uchafu kutoka kwa maji yaliyoganda ya Bahari ya Beaufort huku Kirby akibainisha kuwa: "Hatujui ni kitu cha nani, kiwe cha serikali au kampuni au kibinafsi."

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**MERINA MARCELINO LUAMBANO** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba **TAE 492482** iliyotolewa **DAR ES SALAAM PCO JULY 14 2022 .** Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/58766/2023**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya UBUNGO kituo cha JUMUISHI TEMEKE KATIKA MAHAKAMA INAYOTEMBEA KIBAMBA mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na 22/ 2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ASHURA SEIF wa NYAMWANGI.**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HUSSEIN ISSA CHANZI.**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni ya usimamizi wa mirathi mahakama ya mwanzo**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu ,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo TAREHE 14 Mwezi 2 Mwaka 2023 Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kulete mahakamani kukaguliwa.
Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leo 10 Mwezi 2 Mwaka 2023.

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 14/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU PUDESIANA BENEDICTI LULANGALANGA WA K/ NDEGE KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NAGODFREY VEDASTO FILISIAN**

**TANGAZO**
(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 13 / Mwezi 02 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 08 mwezi 02 mwaka 2023**

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NA. 62/2022**
**HILDA LEMBUKA MWAMKINGA............................MDAI**
**DHIDI YA**
1. **BARAKA KANDONGA............................MDAIWA**
2. **PASCAL MBWILO.................................MDAIWA**
3. **SHADRACK AMANI MWAMKINGA........MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**
**HILDA LEMBUKA MWAMKINGA............................MDAI**
**KWA:**
**PASCAL MBILO,**

Fahamu kwamba HILDA LEMBUKA MWAMKINGA amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 28/02/2023 saa 2.30 asubuhi mbele ya T. Munzerere Mwenyekiti wa Baraza. Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.

Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza ya Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe na mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.
**Kumbuka:** Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 08/02/2023

MAKALA

# USHINDANI WA ELIMU UWE JUU YA UJUZI SI MITIHANI



Na Magabilo Masambu

KWANZA niungane na Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA) kwa uamuzi wake wa kutotangaza shule na wanafunzi bora katika matokeo ya kidato cha nne. Uamuzi huu umeleta maswali na minong'ono mingi katika jamii. Wako wanaodai kwamba ni kwa sababu shule za serikali hazijafanya vizuri, wengine wanasema serikali imekwepa kutangaza shule kwa sababu inahofia kutangaza biashara za waliofaulisha. Hayo inajua serikali, sipo hapa kwa ajili ya kuyajibu.

Natumaini kwamba maelezo yaliyotolewa Februari Mosi bungeni na Waziri mwenye dhamana ya elimu, Profesa Adolf Mkenda, baada ya mwongozo ulioombwa na Mwita Getere, Mbunge wa Bunda Vijijini (CCM), yangetosha kuondoa shaka na maswali mengi miongoni mwetu. Hili jambo la ushindani wa matokeo ya mitihani badala ya ushindani wa maarifa na ujuzi, limeleta matatizo makubwa sana katika elimu yetu. Nimewahi kuandika sana juu ya kusitishwa kwa utaratibu huu.

Katika gezi hili toleo Julai 20-26, 2022 ukurasa wa 13, makala yenye kichwa cha habari "Matokeo makubwa yanavyoumiza" nilieleza athali za kutaka matokeo makubwa katika elimu bila kujali ubora wake katika kujenga fikra, ujuzi na maarifa kwa wahitimu, jinsi yatakavyotoa matokeo mabaya ya wahitimu hao kwa baadaye katika utendaji wao wa kazi katika nyanja mbalimbali.

Msukumo mkubwa sasa uko kwenye matokeo ya mitihani lakini ni wazi kuwa matokeo ya mitihani pekee hayawezi kuwa kipimo sahihi cha ubora wa elimu nchini. Matokeo yanatumika kpima ongezeko au kupungua kwa ufaulu na si ubora. Tutapata watu waliofaulu mitihani lakini wasio na ujuzi kwa sababu tunachotaka jamii isikie ni juu ya ufaulu. Jambo hili linatoa msukumo kwa wamiliki na wakuu wa shule nchini kutumia njia na mbinu mbalimbali za ovyo kuhakikisha shule zao zinasikika kwamba zinafanya vizuri ndiyo maana baada ya kusitishwa kwa jambo hili la kutangaza shule na wanafunzi bora, kelele zimekuwa nyingi maana nia ilikuwa kusikika na si kwa ubora wa elimu wanayoitoa.

Sasa watu wengi hawajui kinachofanyika huko shuleni mpaka shule fulani unasikia wamefaulisha sana. Wengi wanadhani kwamba walimu wanafundisha sana. Kwa sehemu wanafanya lakini si kwa kiwango hicho. Hapa nitaeleza mbinu chache zingine za ovyo kabisa zinazotumika kuhakikisha baadhi ya shule zinajisifu eti na kutembea kufua mbele halafu kwa pamoja tutaona kama ni njia sahihi za kuwafanya waonekane wanafanya kazi au ni tofauti na wengine.

Nitawarejesha nyuma kidogo. Miaka ya zamani kabla ya elimu yetu haijawa biashara kamili na shule zilipokuwa chache, wanafunzi waliokuwa wanaonekana bora ni wale walofaulu na kuchaguliwa katika shule za serikali na wale waliokuwa wanakwenda shule za binafsi walionekana wana uwezo mdogo na kwamba wameshindwa kufaulu vizuri ndiyo maana wamekwenda shule binafsi. Kwa mantiki hiyo, wanafunzi wa shule za binafsi walijiona wanyonge sana na wa shule za serikali walijiona miamba.

Miaka ya hivi karibuni, mambo yakabadilika na hii ni baada ya serikali kujenga shule nyingi za kata ambazo sasa zilikwenda kumeza wanafunzi karibu wote wa shule za msingi. Mbinu ya kwanza ikaibukia hapa, shule za binafsi zikaja na mtindo wa kuchuja wanafunzi ili wachukuwe wazuri maana sasa hakuna mwanafunzi anayefeli mwenye uwezo ambaye atabaki nyumbani ili ajiunge na shule ya binafsi kama ilivyokuwa zamani.

Kwa hiyo wakaja na mtindo wa kufanyisha usaili, wanafanya wanafunzi 300 halafu jamaa anachukuwa wanafunzi watatu waliofanya vizuri. Anakwenda shule nyingine anafanyisha mtihani wanafunzi 200 anachukua wawili waliofanya vizuri. Anafanya hivyo mpaka wanaenea anaohitaji. Tafsiri yake ni kwamba tayari amechukua wanafunzi wenye uwezo binafsi kisha anaweka nguvu kidogo tu halafu akiibuka mshindi, naye anajisifu na kujipongeza kwamba anafanya vizuri! Tena hapo wanaofanya huo usahili ni wanafunzi wa shule binafsi ambao pia wamesoma mchepuo wa Kiingereza.

Mbinu ya pili inayotumika ni kuhamisha wanafunzi. Profesa Mkenda alieleza akitoa mfano kwamba shule yenye wanafunzi 200 ikifanya mtihani 170 wakapata A wanaosalia wale 30 shule inatafuta utaratibu wa kuwaondoa kwa mbinu mbalimbali ili wabaki na 170 watakaowafanya wawe kinara. Wengine wanawafanyisha mtihani wale wale waliochaguliwa hapo, wakishindwa kufikisha ufaulu wanaoutaka, wanawahamisha kama si ubaguzi katika elimu ni nini? Je, jambo kama hili ni sawa lifanyike kwa minajili ya kutafuta matokeo mazuri? Na huu utaratibu unafanyika hata kwenye baadhi ya shule za serikali, ambazo nazo zinataka sifa zisifike kwamba hazifelishi.

Mbinu ya tatu ni kukataa kupokea baadhi ya wanafunzi wanaohamia wenye ufaulu wa chini, yaani nafasi ipo lakini unasema matokeo yake hayaridhishi. Huyu ni Mtanzania, unataka akasome wapi ambako yeye hasitahili kufaulu? Sisi wazazi tunazaa watoto wenye uwezo tofauti tofauti kiakili, lakini pia wanaweza kuwa wengine wana ulemavu fulani kwa hiyo ndiyo kusema kama wana kasoro tuwatenge ili tu watu huko mtaani watuone kwamba hatujazaa watoto wenye kasoro? Tunaona haya yote ni sawa ili tutangazwe sisi ni washindi.

Mbinu zingine ni hizo za kuiba mitihani. Tumesikia kwamba karibu wanafunzi 333 walifutiwa matokeo. Hayo yote yanafanyika ili watu watangazwe wamo 10 bora ili iweje. Na sababu za kufanya hivyo ziko nyingi, baadhi ni kutafuta madaraka ya juu. Mkuu wa shule anataka kuwa ofisa elimu hasa kwa shule za serikali. Kwa upande wa shule za binafsi wanataka wateja waongezeke wafanye biashara ya uhakika.

Ikiwa mtazamo wetu utabadilika sasa, tukawaza namna ya kujenga ujuzi na maarifa bora kwa watoto wetu, tukaondoka huko kwenye ushindani wa matokeo hatutahangaika kuiba mitihani, sjui kuchuja wanafunzi, kuhamisha au kukataa kuwapokea kwa sababu ya ufaulu wao kila mwanafunzi atajifunza na kutoka na alichoelewa. Haya matokeo pia yametumika kupandisha gharama katika elimu nchini hasa shule za binafsi, mtu anafanya ujanja ujanja kama nilioutaja ili asikike, kisha anapandisha gharama za ada halafu ukishindwa kulipa anakwambia shule si hii tu tutafika kweli?

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Siri za ndoa sasa zinatolewa nje, mke hajui kupika, mume anaruka ukuta*



Na Adam Fungamwango

KWA siku za karibuni tumekuwa kwenye baadhi ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii tumeshuhudia migogoro ya ndoa ya baadhi ya watu maarufu nchini.

Kwa bahati mbaya wao wenyewe wamekuwa wanayaweka bayana kwenye vyombo hivyo kuwa gumzo kila kona. Wabongo walikuwa hawajawahi kuona wanandoa wanaitisha mkutano na waandishi wa habari kuelekezea hali ilivyo, au kilichotokea, nini kinaendelea na vingine vinavyofanana na hivyo.

Akiitisha bwana, kesho bibi anaitisha. Na kwa dunia ya sasa ni bando lako tu. Unayaona na kusikia yote. Inawezekana huu ndio mtindo wa maisha ya kisasa kwa watu maarufu kwa sababu dunia imebadilika sana.

Huko nyuma ilikuwa huwezi kusikia kitu kama hicho. Mke na mume wanaachana na sababu zinabaki kwenye vifua vyao. Ndiyo maana haikuwa ajabu sana zamani kuona mume amemuacha mke, halafu baada hata miaka mitatu mpaka mitano wanarudiana tena. Hakuna yeyote aliyeamua kutoka hadharani na kumkandia mwenzake, kumsema vibaya, mbele ya hadhara.

Labda wanaweza kugombana wenyewe ndani na kusemwa kwenye kikao cha usuluhishi lakini yeyote asayehusika hawezi kujua sababu. Majirani na baadhi ya ndugu watabaki na dhana tu pamoja na uzushi, lakini hawatokuwa na sababu halisi iliyosababisha kuachana.

Ugomvi wa wanandoa na vitu vyote vinabaki siri ya ndani kama ambavyo Mwenge Jazz Band wanavyotuambia kwenye wimbo wa 'Tuheshimiane',

mke anashuhudia vituko vya mumewe kila kukicha, lakini badala ya kupiga kelele, anamsubiri mwenyewe na wanakaa wawili na kumwambia.

"Kama unaweza kuamua toka sasa, nambie waziwazi mpenzi wangu, usiwe na shaka kuwa nitachukua, hata mimi naelewa ni kidunia, tuachane kwa wema, mama aaa, ili tukija tengana popote pale, tusabahiane, ikiwezekana, turudiane. Nimeamua kubadili tabia sababu ni wewe mwenyewe, vitendo unavyovifanya na siri zako zote nimezipata, nikisema niseme hautachukia?

"Umenifanya nidharauliwe na wasichana wako, umenifanya nidharauliwe na marafiki zako, na hadhi yangu imeshuka, heshima imepungua, popote pale nipitapo. Kama kweli unanipenda badili tabia yako we bwana."

Haya ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo, mwanamama akimpasha kwa hekima mumewe juu ya kile ambacho anamfanyia.

Hajamjia juu kama moto wa kifuu, maana kuna kinamama hapo mumewe kafanya kosa kidogo utasikia.

"Usinibabaishe bwana, unafikiri sina kwetu, sijaua mimi nyumbani, kwanza katika wanaume wewe naye mwanaume?"

Maneno haya badala ya kutibu tatizo na kusuluhisha mgogoro, huwa yanachochea mara mbili ya matatizo yaliyokuwapo. Muhimu ni masikizano.

Mwanamume naye kutoa maneno ndani kupeleka nje ni tatizo kubwa. Wanaume wenyewe huwa wanasema tatizo hili lipo sana kwa akinamama. Kwa sasa wanaume nao wamekuja juu. Nao hawana kifua cha kuhifadhi vitu. Nao wanatoka na kwenda kutoa siri za ndani nje.

Vijana Jazz Band waliliona hili katikati ya miaka ya 1990. Nadhani walikuwapo wanaume wachache sana wenye tabia hili. Wakalikemea kwa wimbo wa 'Siri ya Ndani'.

"Mume wangu nakueleza, mume wangu nasikitika kwa tabia yako ya kushindwa kunieleza nikukoseapo. Si tabia nzuri eee, tabia ya umbea nitashindwa nakueleza mwanaume hawi hivyo mume wangu. Ninapokosa nirekebishe mkeo, ndiyo tunavyoishi hapa nyumbani.

"Siri ya ndani ni siri ya ndani bwana ee, siri ya mtungi ajuae kata ee, ninapokukosea, nieleze, ili na mimi nipate kujirekebisha ee."

Huyu bibie anampasha mumewe kwa tabia ya kushindwa kumweleza anapomkosea, badala yake anakwenda vijiweni na sehemu zingine kwa marafiki zake na kumsema mkewe, akitoa siri za ndani, au watoto wa mjini wanasema siri za kambi.

"Mimi na wewe kwa nini tunakosana, tukae chumbani na kuyamaliza, sasa inakuwaje unakwenda kuyatoa nje. Unanilaumu eti mimi sijui kupika, wakati kosa hilo ni lako mume, unaleta unaleta kauzu halina nyanya wala kitunguu, unaleta mchele bila nazi, wala mafuta."

Mwanamume huyu akienda kula huko kwa rafiki zake, anawaambia mkewe hajui kupika. Sasa mke anampasha kwa kumwambia yeye kupika anajua, tatizo ni mbahili, analeta mboga bila viungo vyake ambavyo vinaleta ladha nzuri kwenye mboga na hata akinunua mchele, unakuwa hauna nazi wala mafuta, wali unapikwa hivi hivi kwa hiyo hauwezi kuwa na ladha nzuri. "Chakula kitamu viungo babu we. Ndivyo wimbo wa Vijana Jazz unavyoendelea kwenye ubeti wa mwisho.

"Mbona wewe siri zako najaribu kuficha, hodi hodi kila siku watu kuja kudai madeni, wala ujificha uvunguni, siku nyingine mume we, unaruka ukuta."

Mke anamkumbusha hata yeye ana matatizo kibao, lakini hajakaa na mashoga zake kuwaelezea kuwa ana madeni kila kona, madukani na sehemu zingine kiasi mpaka wadai wanafika nyumbani. Mume sasa analazimika kujificha uvungumi ili wasimwone, lakini siku nyingine akiona hali inaweza kuwa mbaya na wakamsaka hadi uvunguni, akaruka ukuta wa nyumba na kukimbia ili wanaomdai wasimkute au kumuona."

# HADITHI

# Harusi Imevunjika-18

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi, Jerry Mohamed, aliliongoza kundi la ndugu, jamaa na marafiki kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaj, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele.

Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea na kwa nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

**************************************




Jerry aliangua tena kicheko. Lakini hakikuwa halisi.

"Sahau kuhusu hilo. Haiwezekani na haitowezekana. Mimi si mjinga kiasi hicho. Mtu akufanyie vile mbele ya watu wote unaowaheshimu na wanaokuheshimu, halafu tena umweke ndani kwako. Wote waliokuwa kwenye harusi siku hiyo wakija kukutembelea nyumbani kwako wamkute, liwe simulizi mitaani?

"Sawa, ila usimwambie kama nimekupigia simu tumeongea."

"Kwanza mimi nina muda naye? Sijawahi kuongea naye hata siku moja tangu alipoondoka. Kuna siku kama mbili tatu hivi tena hizi hizi za karibuni alikuwa ananipigia visimu vyake, mimi nikiona ni yeye sipokei na akatuma meseji sijajibu. Hajatuma tena."

"Sawa Shem, maana..."

"Zulfa usiwe na wasiwasi, nitakachokuja kufanya huko na kuamua, hatokugusa au kukuuliza kitu tena kuhusu mimi."

Majibu hayo yalionekana kumfurahisha na kumfariji Zulfa. Hakujua ni nini hasa Jerry atakuja kusema lakini alikuwa na uhakika kuwa suala la Jerry kumrudia tena dada yake halipo. Hilo ndilo lilimfurahisha zaidi. Hata yeye mwenyewe hakujua ni kwa nini. Kutokana na furaha iliyomjaa moyoni akaazimia kuwa hatomjibu chochote dada yake. Atakaa kimya kama mjinga, akimsubiri Jerry aamue atakafanya.

Mambo yalionekana kuwa magumu kwa Vayajo. Alikwenda kwa rafiki yake Nasma kwa ajili ya kumpeleka kwa mganga wa kienyeji. Walifika na mganga alizidi kutia chumvi kwenye kidonda chake kilichokuwa kibichi kabisa. Tayari alikuwa amemsimulia kila kitu, hivyo mganga alichokuwa akifanya kuchezesha dishi tu.

"Duuh, huyo mdogo wako ni mtu mbaya sana. Hapa kwenye kioo changu kinanionyesha kuwa ni kweli, ana uhusiano wa kimapenzi na huyo aliyetaka kukuoa. Na mpaka sasa wanapendana na wanaendelea na mapenzi yao kwa siri. Kwa hiyo mteja ukizubaa mdogo wako atakuzidi kete. Yeye ndiye ataolewa na mwanamume huyo baadaye."

Maneno hayo yalionekana kumshtua zaidi Vayajo kwani kwake awali ilikuwa dhana tu, lakini anathibitishiwa na mganga.

"Sasa unataka kufanya nini mteja?" Akauliza mganga.

"Nachotaka mimi ni kwamba, mdogo wangu atokee tu ghafla kumchukia Jerry na mwenyewe Jerry moyo wake uwe mweusi kwa Zulfa, halafu arudi tena kunipenda mimi, halafu arudishe moyo anioe."

> **"Nachotaka mimi ni kwamba, mdogo wangu atokee tu ghafla kumchukia Jerry na mwenyewe Jerry moyo wake uwe mweusi kwa Zulfa, halafu arudi tena kunipenda mimi, halafu arudishe moyo anioe."**

"Sawa, basi ngoja kiti apande, halafu akikuuliza utasema dhamira yako au unachokihitaji." Akamaliza mganga na akaanza kutikisa kichwa na kutetemeka kama mtu aliyekunywa au kunyweshwa dawa chungu. Baadaye mwili mzima sasa ukaanza kutetemeka na kuanza kuongea maneno yasiyoeleweka vyema.

"Kanga na bata mzuri, mzuri kanga, kanga na kuku mzuri nani, mzuri kanga, kanga na mbuni mzuri nani mzuri kanga.

Kaduli twanga kaduli twanga, kula wewe simba mwitu wa hiari. Napata habari juzi juzi nalisikiza Usevya kuna mambo, mzee mmoja alipita Lyamba lya Mfipa mlima kauvamia vibaya msitoe machozi, yuko kijana mmoja katokea mbali Urwila wamemchinja kama sokwe. Ndugu zake hawajakubali, leo mtaona, leo mtaona, leo mtaipata..."

Wimbo huo uliimbwa na mganga Mbomvya kwa ustadi na kila alipokuwa akiendelea alikuwa akiuimba kwa haraka zaidi na sauti ikawa inaongezeka na kuwa ya kutisha baadaye alitulia. Akaanza kuyumbayumba na kuuliza nini ambacho mteja anahitaji.

"Nataka ndoa. Nataka mpenzi wangu ambaye alitaka kunioa, sasa anioe. Nataka asiwe tena na uhusiano na mdogo wangu Zulfa. Nataka Zulfa naye asimpende tena mchumba wangu Jerry."

"Ahaa, yote yatatimizwa, sema tawile."

"Tawile mganga."

Mganga Mbomvya alipunguza utetemaji wake na baadaye akatulia kimya. Akaonekana kama mtu ambaye anashangaa kitu na aliyechoka mwili.

"Tayari nadhani kila kitu kimekwenda sawa, umeshaelewana na mgeni aliyekuja?"

"Ndiyo, nimeelewana naye."

"Basi sasa, nitakupa dawa na masharti ambayo unatakiwa kuyafuata ili afanye kazi kwa haraka." "Sawa nimeelewa mganga."

Vayajo alitoka kwa mganga na furaha moyoni. Tayari kila kitu kiko mikononi mwake. Ni utekelezaji tu ndio unaotakiwa kufanywa. Unatakiwa kufanywa kwa uangalifu.

Alirudi nyumbani na kumsalimia mdogo wake. Akamsalimia kwa mbwembwe na bashasha, akionekana mwenye furaha. Hili lilimshtua na kumshangaza Zulfa.

Ni mwezi sasa umepita hawasalimiani wala kuongea. Kuongea kwao ni lawama, ugomvi na kutafutiana visa. Mama yao ameongea weee, mwisho kaamua kuwatazama macho. Alichoshukuru ni kwamba tu hawaparurani. Zulfa alijibu salamu ya dada yake, ingawa kwa kuchelewa.

Hakujua ni nini kilichomfanya dada yake kuwa na furaha wakati wamekasirikiana. Akili yake ikarudi kwa Jerry.

Akadhani huenda wamepatana na Jerry.

Zilibaki siku mbili tu ambazo Jerry alisema kuwa atakwenda kijijini Msangani. Zulfa akaona ni mbali sana kusubiri. Kwanza alitaka akae kimya na kuja kumuuliza akiwa pale. Lakini hakupata usingizi. Mwenyewe hakujua ni kwa nini.

Akampigia simu shemeji yake Jerry.

"Nachoshangaa kuanzia jana, da' Vayajo anavyonisalimia kwa bashasha kama vile hatukuwahi kugombana, limenishangaza, nikaona nikupigie huenda mmeshaelewana, mimi tena nisije kuonekana mgombanishi."

"Hapana, mwenyewe anajua sababu inayomfanya hivyo, ila sijaongea naye chochote kile. Lakini Zulfa kwa hilo unaloniambia, kuwa makini sana naye leo na kesho. Inavyoonekana kuna kitu kinampa matumaini. Nakutumia pesa hapa, usinywe maji ya kwenye mtungi kwenu na kama unakula chakula basi kula cha familia nzima, usile kitu chochote cha peke yako. Kesho kutwa mimi nakuja, sawa?"

"Sawa." Akajibu na kurejea kwenye hali ya furaha kama mwanzo.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# RAPA AKA AUAWA KWA RISASI SAUZI

Rapa Kiernan Forbes mwenye umri wa miaka 35 anayefahamika kwa jina la AKA ameuawa kwa kupigwa risasi juzi nchini Afrika Kusini.

Polisi nchini humo wamethibitisha kuwa mwanamuziki huyo mwenye miaka 35 alipigwa risasi sita nje ya ukumbi wa burudani Ijumaa usiku kwenye barabara ya Florida jijini Durban.

Habari zinasema kuwa mara baada ya tukio hilo, polisi walionekana kuzingira eneo hilo, huku wateja waliokuwa kwenye eneo hilo wakipigwa butwaa kwani awali walimuona rapa huyo akiwa amesimama nje kabla ya kupigwa risasi.

Polisi wamesema kuwa barabara ya Florida imefungwa baada ya tukio hilo, ambapo watu wawili akiwemo rapa huyo wamethibitioshwa kufariki.

Rapa huyo ambaye pia ni mwandishi wa nyimbo, mwimbaji, mwigizaji, mtaalam wa sauti na produzya alizaliwa Januari 28 1988 kwenye jiji la Cape Town nchini humo.

Ameshawahi kutoa ngoma kibao ambazo zilihiti kinoma, lakini atakumbukwa kuwa alishawahi kutoa ngoma moja akimshirikisha Diamond Patnumz, bonge moja la kolabo lililopewa jina la 'Make Me Sing.'

## ZISIKUPITE

### MADDISON ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur ni miongoni mwa timu zinazovutiwa na kiungo wa kati wa Leicester City na Timu ya Taifa ya England, James Maddison, 26. (***Mirror***)

### SPURS: KANE HAONDOKI

TOTTENHAM Hotspur haitamruhusu, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29 kujiunga na mpinzani wao wa Ligi Kuu England, msimu huu - bila kujali bei - huku klabu za Manchester United na Bayern Munich zikimnyatia mshambuliaji huyo. (***90 min***)

### LUKAKU, PULISIC KUUZWA

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 24, ni miongoni mwa wachezaji ambao huenda wakauzwa na Chelsea pamoja na winga wa Morocco, Hakim Ziyech (29) na mshambuliaji wa Ubelgiji Romelu Lukaku (29), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Inter Milan. (***ESPN***)

### MILAN YAMFUATA BALOGUN

AC Milan ya Italia inatazamia kufufua nia yao ya kumnunua mshambuliaji wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England, Folarin Balogun mwenye umri wa miaka 21. (***Mail)***

### KEITA ANUKIA MILAN

KLABU ya AC Milan pia wanamtaka kiungo wa kati wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Guinea, Naby Keita mwenye umri wa miaka 27. (***Mirror***)

### TAH KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL na Newcastle United zinatajwa kuvutiwa na beki wa kati wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Jonathan Tah, mwenye umri wa miaka 26. (***90min***)

### SABITZER NEEMA YAJA

KLABU ya Manchester United iko tayari kumsajili kiungo wa Austria, Marcel Sabitzer, mwenye umri wa miaka 28 kwa mkataba wa kudumu ifikapo msimu wa joto ikiwa atavutia wakati wa kipindi chake cha mkopo kutoka Bayern Munich pale Old Trafford. (***ESPN***)

### SPURS KUMSAJILI BRAZ

KLABU ya Tottenham Hotspur huenda ikamnunua kinda wa Benfica, Rui Pedro Braz. (Mirror)

### AUBAMEYANG AWEKA MGOMO

MSHAMBULIAJI wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 33, atasusia kuhamia Los Angeles FC na kupigania nafasi yake katika kikosi cha Chelsea. (***Telegraph***)

### FATI AGOMBEWA EPL

MANCHESTER United, Arsenal na Liverpool zote zimefanya mazungumzo na wakala wa mshambuliaji wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania, Ansu Fati, mwenye umri wa miaka 20. (***Fabrizio Romano***)

### UNITED YAMTAKA VERMEEREN

KLABU ya Manchester United pia inamfuatilia kiungo wa kati wa Royal Antwerp na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Arthur Vermeeren, mwenye umri wa miaka 18. (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI, BENZEMA, MBAPPE WACHUANA

## Ni katika kuwania tuzo ya Mchezaji Bora wa FIFA itakayotolewa...

**PARIS,** Ufaransa

WACHEZAJI, Karim Benzema, Lionel Messi na Kylian Mbappe wameingia katika tatu bora ya kinyang'anyiro cha kumtafuta Mchezaji Bora wa mwaka 2022 wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Baada ya kutangaza orodha ya mwisho ya makocha watakaowania tuzo ya kocha bora wa mwaka, FIFA imewatangaza wachezaji hao wanawania tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa kiume.

Orodha hiyo imeongozwa na Benzema, Messi na Mbappe.

Wachezaji hao wamefanikiwa kuingia kwenye kinyang'anyiro hicho baada ya kufanya vizuri zaidi mwaka jana na kuzisaidia timu zao kutwaa mataji mbalimbali.

**Benzema alifanikiwa kuchukua tuzo ya Ballon Dor akiisaidia Real Madrid kutwaa taji la Laliga na Ligi ya Mabingwa Ulaya huku akiibuka Mfungaji Bora.**

Messi yeye alifanikiwa kutimiza ndoto yake ya muda mrefu baada ya kufanikiwa kuiwezesha Timu ya Taifa ya Argentina kubeba Kombe la Dunia katika fainali zilizofanyika Qatar.

Huku akifanikiwa kunyakua tuzo ya mchezaji bora wa michuano hiyo, lakini pia klabu yake ya PSG aliiwezesha kutwaa taji la Ligi Kuu Ufaransa.

Mbappe kwa upande wake alifanikiwa kuwa na mwaka mzuri sana akiisaidia PSG kunyakua taji la Ligi Kuu Ufaransa huku akimaliza kama Mfungaji Bora wa ligi hiyo.

Mbappe pia aliisaidia Timu yake ya Taifa ya Ufaransa kufika fainali ya Kombe la Dunia na kuibuka Mfungaji Bora wa michuano hiyo.

Tuzo hizo zinatarajia kutolewa katika sherehe maalumu itakayofanyika Februari 27, mwaka huu.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 472,

MECHI KALI
LEEDS
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 3.53
X | 3.58
2 | 1.93

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ANTONY, MARTIAL KUIKOSA BARCELONA



**MANCHESTR,** England

WACHEZAJI wa Manchester United, Anthony, Martial na Scott Mctominay wanaelezwa wako katika wasiwasi wa kuukosa mchezo wa Kombe la Europa dhidi ya Barcelona.

Kocha wa Manchester United, Erik Ten Hag, amewaambia waandishi wa habari kuhusu kurejea kwa wachezaji hao katika mtanange dhidi ya Barcelona utakaochezwa Alhamisi na kusema hana uhakika kwa asilimia 100, lakini alisisitiza hatarajii hilo kutokea.

United imeanza kuandamwa na majeruhi, kiungo wake, Donny Van De Beek ni majeruhi na atakosekana kwa msimu mzima uliobakia.

Lakini siku chache zilizopita aliumia kiungo, Christian Eriksen ambaye atakua nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu.

Pia wachezaji Antony, Martial, na Mctominay wamekua wakiandamwa na majeraha ya hapa na pale.

Antony yeye alipata majeraha katika mchezo wa Ligi Kuu England wikendi iliyopita dhidi ya Crystal Palace wakati Martial na Mctominay wao waliumia siku kadhaa nyuma na wataendelea kukosekana katika michezo inayofuata.

# Guardiola: Nitabakia City



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema ataendelea kubakia ndani ya klabu hiyo licha ya tuhuma ambazo anakabiliwa nazo kwa sasa.

Guardiola amezungumza na wanahabari na kuzishutumu klabu pinzani katika Ligi Kuu England na kusema wapo nyuma ya mashtaka ambayo yanawakabili.

Lakini baada ya kuzungumza hayo alisisitiza anataka kuendelea kuwatumikia matajiri hao wa jiji la Manchester.

Kocha huyo amesema timu 19 katika ligi hiyo zilikua zinataka City iadhibiwe kipindi ambacho ilishtakiwa kwa kuvunja utaratibu wa matumizi ya fedha na Shirikisho la Soka la Ulaya (UEFA).

Lakini kocha huyo amesema anaamini klabu hiyo haijavunja utaratibu na wataondolewa katika mashtaka yao ya sasa.

Pia makocha wamekua wakiwaajiri ndani ya klabu hiyo kitu ambacho kinaweza kuwagharimu kwa kiwango kikubwa ikithibitika ni kweli juu ya tuhuma hizo.

,189,430

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/02/23 | 20:00 | Omonia Nicosia vs Apoel Nicosia | 2.55 | 3.16 | 2.55 |
| 02. 15/02/23 | 22:30 | Arsenal vs Manchester City | 2.71 | 3.24 | 2.48 |
| 03. 15/02/23 | 22:45 | Motherwell vs St Mirren | 2.36 | 3.23 | 2.93 |
| 04. 15/02/23 | 22:45 | Preston vs Luton Town | 2.53 | 3.13 | 2.73 |
| 05. 15/02/23 | 23:00 | Borussia Dortmund vs Chelsea | 2.37 | 3.37 | 2.77 |
| 06. 16/02/23 | 06:05 | Club Necaxa vs UNAM Pumas | 2.45 | 3.35 | 2.71 |
| 07. 16/02/23 | 20:45 | RB Salzburg vs Roma | 2.73 | 3.23 | 2.53 |
| 08. 16/02/23 | 20:45 | Sporting Braga vs Fiorentina | 2.43 | 3.39 | 2.74 |
| 09. 16/02/23 | 23:00 | Sevilla FC vs PSV Eindhoven | 2.24 | 3.39 | 3.05 |
| 10. 16/02/23 | 23:00 | Sheriff Tiraspol vs Partizan | 2.50 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 17/02/23 | 00:00 | Mirassol SP vs Ituano SP | 2.68 | 2.89 | 2.63 |
| 12. 17/02/23 | 03:30 | Corinthians vs Palmeiras | 3.00 | 2.75 | 2.24 |
| 13. 17/02/23 | 11:45 | Western United vs Wellington Phoenix | 2.70 | 3.23 | 2.53 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAPILI - 12/02/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 3122 | Sparta Rotterdam vs GO Ahead Eagles | 1.99 | 3.27 | 3.67 |
| 14:30 | 4001 | Udinese vs Sassuolo | 2.03 | 3.41 | 3.41 |
| 15:00 | 1553 | Toulouse vs Rennes | 2.93 | 3.32 | 2.31 |
| 15:00 | 1731 | Mohammedan SC vs Gokulam Kerala FC | 2.13 | 3.12 | 3.22 |
| 15:00 | 5218 | Frosinone Youth vs AC Milan Youth | 2.07 | 3.41 | 3.10 |
| 15:30 | 4285 | Racing Genk vs Royal Antwerp | 1.97 | 3.48 | 3.58 |
| 16:00 | 3994 | Getafe vs Rayo Vallecano | 2.85 | 2.75 | 2.80 |
| 16:00 | 5558 | Ihefu FC vs Singida BS FC | 2.42 | 2.60 | 2.90 |
| 16:15 | 1234 | FC Lugano vs FC Luzern | 2.43 | 3.34 | 2.75 |
| 16:15 | 1915 | AC Bellinzona vs FC Schaffhausen | 2.14 | 3.41 | 2.95 |
| 16:30 | 2109 | SCR Altach vs LASK Linz | 4.25 | 3.63 | 1.70 |
| 16:30 | 2333 | Heerenveen vs Feyenoord | 4.55 | 3.71 | 1.69 |
| 16:30 | 4643 | Josko Ried vs TSV Hartberg | 2.05 | 3.32 | 3.21 |
| 16:30 | 4703 | Vitesse Arnhem vs Utrecht | 2.43 | 3.38 | 2.69 |
| 17:00 | 1283 | Reims vs Troyes | 1.52 | 4.18 | 5.58 |
| 17:00 | 1853 | Sigma Olomouc vs Hradec Kralove | 1.87 | 3.61 | 4.04 |
| 17:00 | 1966 | Montpellier vs Brest | 2.36 | 3.34 | 2.84 |
| 17:00 | 2425 | Dundee FC vs Cove Rangers | 1.40 | 4.50 | 6.70 |
| 17:00 | 3171 | Mlada Boleslav vs Pardubice | 1.53 | 4.30 | 5.80 |
| 17:00 | 3907 | Leeds vs Manchester Utd | 3.53 | 3.58 | 1.93 |
| 17:00 | 4636 | Lille vs Strasbourg | 1.46 | 4.28 | 6.36 |
| 17:00 | 4661 | Juventus Youth vs Sassuolo Youth | 1.88 | 3.57 | 3.47 |
| 17:00 | 5474 | Bologna vs Monza | 2.18 | 3.17 | 3.27 |
| 17:00 | 5576 | Angers vs AJ Auxerre | 2.26 | 3.34 | 2.99 |
| 17:00 | 5920 | Viseu vs Sporting Farense | 2.19 | 3.26 | 3.11 |
| 17:30 | 2723 | Hertha BSC vs Monchengladbach | 2.73 | 3.42 | 2.38 |
| 18:00 | 1979 | Anderlecht vs St Truiden | 1.91 | 3.44 | 3.84 |
| 18:15 | 3486 | Real Oviedo vs Burgos | 2.15 | 2.88 | 3.72 |
| 18:15 | 3736 | Celta Vigo vs Atletico Madrid | 3.40 | 3.10 | 2.20 |
| 18:30 | 1585 | Famalicao vs Gil Vicente | 2.17 | 3.28 | 3.23 |
| 18:45 | 2849 | Twente vs FC Volendam | 1.23 | 5.96 | 9.94 |
| 18:45 | 5215 | Ajax vs Waalwick | 1.12 | 8.15 | 14.91 |
| 19:00 | 2131 | Austria Vienna vs Austria Klagenfurt | 1.86 | 3.57 | 3.52 |
| 19:00 | 2242 | Rangers vs Partick Thisle | 1.11 | 7.07 | 16.64 |
| 19:05 | 5801 | Nantes vs Lorient | 1.97 | 3.43 | 3.63 |
| 19:30 | 3101 | Manchester City vs Aston Villa | 1.26 | 5.52 | 9.79 |
| 19:30 | 4587 | FC Koln vs Eintracht Frankfurt | 2.63 | 3.38 | 2.47 |
| 20:00 | 2830 | Juventus vs Fiorentina | 1.88 | 3.35 | 4.03 |
| 20:30 | 2781 | Eibar vs FC Cartagena | 1.71 | 3.41 | 4.94 |
| 20:30 | 4119 | Valladolid vs Osasuna | 2.74 | 2.99 | 2.69 |
| 20:30 | 5275 | Sporting Gijon vs Huesca | 1.89 | 3.07 | 4.45 |
| 20:30 | 5636 | Standard Liege vs Kortrijk | 1.65 | 3.99 | 4.59 |
| 21:00 | 1360 | Aris Salonica vs Panathinaikos | 2.86 | 2.91 | 2.62 |
| 21:00 | 4798 | Voluntari vs Steaua Bucuresti | 3.80 | 3.38 | 1.92 |
| 21:00 | 5885 | Sporting Lisbon vs Porto | 2.64 | 3.23 | 2.59 |
| 22:45 | 2877 | Lyon vs Lens | 2.35 | 3.38 | 2.83 |
| 22:45 | 5213 | Napoli vs Cremonese | 1.17 | 6.75 | 12.90 |
| 23:00 | 3150 | Villarreal vs Barcelona | 3.92 | 3.64 | 1.85 |
| 23:00 | 5813 | UD Ibiza Eivissa vs Ponferradina | 2.33 | 2.98 | 3.17 |
| 23:30 | 1749 | Maritimo vs Sporting Braga | 5.18 | 3.93 | 1.59 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# OPPA, SHIKANGWA TISHIO LIGI KUU YA WANAWAKE

**Na Adam Fungamwango**

MASTRAIKA wa Simba Queens, Jentrix Shikangwa na Oppa Clement (pichani), wameonekana kuwa moto katika kupachika mabao kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ambayo inaendelea katika viwanja mbalimbali hapa nchini.

Mpaka sasa Oppa mwenye mabao tisa ndiye kinara wa ufungaji huku Shikangwa ambaye pia anaichezea Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake Kenya (Harambee Starlets), akiwa na magoli saba. Mastraika hao wawili, wote wakifunga bao moja kila mmoja, Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam dhidi ya Baobab Queens, Simba Queens ikishinda mabao 4-1, huku la Shikangwa akifunga kutokana na 'assist' ya Oppa.

Shikangwa ameonekana mpinzani zaidi kwenye kinyang'anyiro cha kusaka kiatu cha dhahabu huku akiwa amesajiliwa kipindi cha dirisha dogo na kwa muda mfupi tu amefikisha idadi hiyo ya mabao.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu ya Wanawake, nafasi tatu inashikiliwa na Winfrida Charles wa Alliance Girls mwenye mabao sita, huku straika Mnigeria wa Yanga, Blessing Nkor, mchezaji mwingine wa kimataifa wa Kenya, Cynthia Musungu wa Fountain Gate Princess na Mtanzania Fatuma Mustapha wa JKT Queens, wote hao wamepachika mabao matano.

Donisia Minja wa JKT Queens yeye ana mabao manne mpaka sasa kwenye orodha ya wafungaji kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 10.

Simba Queens iko kileleni katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 19 huku Mkwawa Queens yenye pointi moja inaburuza mkia, kila timu imecheza michezo tisa.




# Yanga kuwamaliza Watunisia mapema

INATOKA UK 24

aliliambia gazeti hili wachezaji wote wako tayari kupeperusha vyema bendera ya timu yao na wanachosubiri ni muda wa kufanya kazi ufike.

Mayele alisema wanafahamu wametumwa na wanachama na mashabiki wa Yanga kusaka matokeo mazuri. "Tulipotua tulifanya mazoezi magumu kidogo kwa sababu tunajua mechi itakuwa na kasi kubwa na ilikuwa lazima tujiandae vizuri, tunamshukuru Mungu kila kitu tumemaliza salama, tunasubiri mechi tu tufanye kazi ambayo tumetumwa na Wana-Yanga," alisema Mayele.

Wakati huo huo, Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema wameongeza bonasi kwa wachezaji wao kuelekea mchezo huo ili kuongeza hamasa ya kupata ushindi.

"Tumeongeza zawadi kwa wachezaji wetu, hii ni kuongeza morali na kufanya vizuri katika mchezo wetu wa kesho (leo) dhidi ya wenyeji wetu US Monastir," alisema Hersi.

Hata hivyo, Hersi hakuwa tayari kutaja kiasi cha fedha watakachowapa nyota wa Yanga endapo watavuna pointi tatu za ugenini.

Mechi nyingine ya Kundi D itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya TP Mazembe dhidi ya Real Bamako ya Mali.

Baada ya mechi ya leo, Yanga itarejea nyumbani kuwasubiri TP Mazembe katika mchezo wa pili wa kundi hilo utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Michezo**

**Nipashe**

Jumapili Februari 12, 2023



**Guardiola: Nitabakia City**

UKURASA 22

# Yanga kuwamaliza Watunisia mapema

## ●●● Wachezaji waahidiwa donge nono endapo watapata ushindi katika...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wanatarajia kuwakabili US Monastir katika mechi ya Kundi D ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Olympique Hamadi Agrebi Rades ulioko katika jiji la Tunis, Tunisia.

Mechi hiyo itafanyika kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania.

**Yanga iliyohamia michuano hiyo baada ya kuondolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imepania kuitemesha tena Tunisia kama ilivyofanya Novemba 9, mwaka jana pale ilipoiadhiri Club Africain na kutinga hatua ya makundi.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema maandalizi yote kuelekea mechi hiyo yamekamilika na wachezaji wako fiti kwa ajili ya kupambana kusaka matokeo mazuri.

Kaze alisema wamejipanga kucheza soka la kiwango cha juu na kutafuta mabao ya mapema ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kumaliza mchezo huo wakiwa na ushindi.

"Tumemaliza maandalizi, lakini tuliamua kuwapata wachezaji mazoezi magumu kwa sababu tunajua mechi itakuwa ngumu na ya kasi kutokana na aina ya wapinzani wetu walivyo, wachezaji wote wanajua kama mechi ya kwanza ni muhimu kupata ushindi katika hatua hii ya makundi. Katika mechi tano ambazo unacheza za makundi, mechi ya kwanza ukishinda inakupatia vitu vingi, ukiacha pointi tatu ambazo unapata, pia inakupatia kujiamini kuelekea mechi zinazofuata," alisema Kaze.

Aliongeza wanafahamu wenyeji wao pia wamejipanga kuzibakisha pointi nyumbani, hivyo wataongeza umakini katika safu ya ulinzi na hatimaye kuwabana wapinzani wao.

Alisema safu ya ushambuliaji katika mechi hiyo itaongozwa na Fiston Mayele na Kennedy Musonda ambao wamepewa mbinu mbalimbali za kuwasumbua mabeki wa wapinzani wao kati na kupata njia rahisi ya kumfunga.

"Nimepata bahati ya kuwasoma wapinzani wake na kuona udhaifu na ubora wao, ninataka kuona washambuliaji wanacheza kwa kasi ambao itawasumbua mabeki, tunaweza kupata matokeo mazuri endapo wachezaji watashirikiana vizuri na kujituma, kila mmoja anajua mechi haitakuwa rahisi kwa sababu kuna ubora tunatakiwa kuwa nao," alisema Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi.

Naye straika tegemeo wa Yanga kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Mayele,

INAENDELEA UK 23



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele. **PICHA: MTANDAO**

## Azam FC kuzima moto wa Simba

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umeweka wazi wanahitaji ushindi katika kila mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyosalia na hawatakuwa na hofu ya kuikabili Simba ambayo inatoka kwenye joto la michezo ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imeelezwa.

Azam FC inatarajia kukutana na Simba katika mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Februari 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabiti Zakaria (Zaka), alisema wamejipanga kuendeleza ubabe dhidi ya Simba ili kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoelekea ukingoni.

Zaka alisema malengo yao kwa sasa ni kuona wanamaliza msimu wakiwa katika nafasi tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo kwa sasa mabingwa watetezi, Yanga ndio vinara.

"Tunaendelea kujipanga, bado msimu haujamalizika, malengo yetu makubwa ni kuhakikisha tunafanya vizuri katika kila mechi iliyopo mbele yetu, na tutaanza na mchezo dhidi ya Simba, tunajuwa bado watakuwa na joto la mashindano ya CAF," alisema Zaka.

Aliongeza ili kuhakikisha wanakua imara, wachezaji wao wanafanya mazoezi kila siku na jana walicheza mechi ya kirafiki dhidi ya KMKM FC kutoka Zanzibar.

"Malengo makubwa yalikuwa ni ubingwa, lakini tumeshindwa kuyafikia, sasa tunahitaji kutafuta matokeo chanya kila mechi na mchezo ujao tutacheza dhidi ya Simba, kikubwa tunahitaji alama muhimu ili kuendelea kubaki katika nafasi ya tatu," Zaka alisema.

Aliongeza wanahitaji sana kuendelea kubaki katika nafasi hiyo ambayo pia inawaniwa na Singida Big Stars ili kumaliza msimu kwa heshima.

Azam FC ilitolewa mapema katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika na inahitaji kumaliza katika nafasi ya tatu ili kupata tiketi ya kushiriki michuano ya CAF msimu ujao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >